
SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



RIPOTI MAALUM
**Kitendawili** cha usalama mahabusi walioko polisi-2 UKURASA 4



UKURASA 22

# Nipashe

Jumanne Desemba 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580801

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Magereza yaelemewa

• **Idadi** ya mahabusi yazidi ya wafungwa...*Endelea Uk.2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### JK AELEZA UMUHIMU UHUSIANO KIMATAIFA

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete, ameeleza umuhimu wa Tanzania kujenga uhusiano mzuri na mataifa mengine duniani...

UKURASA WA 3

### POLISI ILIVYOUA 5 MADAI MAJAMBAZI

WATU watano wanaosadikiwa kuwa ni majambazi wameuawa katika majibizano ya risasi na polisi mkoani Kigoma wakati...

## Mamia wataabika usafiri, nauli zapanda

UKURASA 3




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi na Mkurugenzi wa Jubilee Life Insurance, Karim Jamal, wakitia saini mkataba wa ushirikiano na kuzindua rasmi mpango wa bima kwa ajili ya watu wa kipato cha kati na wafanyabiashara, uitwao NMB FANAKA PLAN, jana jijini Dar es Salaam. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Idara ya Bima NMB, Martine Massawe (kulia), Mkuu wa Idara ya Bima kwa Benki wa Jubilee Life Insurance, Dereck Rwezaura (kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**



## Hatima sare JWTZ kesi ya kina Mbowe Januari

UKURASA 2

**MICHEZO** **PABLO APEWA RUNGU SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Magereza yazidiwa mahabusi

Na Gwamaka Alipipi

JESHI la Magereza limewasilisha changamoto nne zinazowakabili kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ambazo zinapaswa kutatuliwa haraka, kubwa ikiwa ni uwapo mahabusi wengi kuliko wafungwa kwenye magereza nchini.

Limeeleza kuwa kwa sasa kuna mahabusi 16,000, huku idadi ya wafungwa ikiwa 14,000 na kusababisha magereza kuelemewa.

Kamishna Jenerali wa Magereza, Suleiman Mzee, alimweleza Waziri Simbachawene jana baada ya kuweka jiwe la msingi na uzinduzi wa miradi mbalimbali ya Jeshi la Magereza mkoani Dar es Salaam.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni uhaba wa askari, kutolipwa posho, pamoja na uvamizi wa maeneo ya magereza unaofanywa na baadhi ya watendaji wa serikali wakiwapa wafanyabiashara.

Kwa mujibu wa Mzee, mahabusi wengi wanakaa kwenye magereza pasipo kesi zao kusikilizwa hali inayosababisha ufinyu wa maeneo ya kuwahifadhi.

**POSHO ASKARI**

Meja Jenerali Mzee alisema kuna changamoto ya muda mrefu ya posho kwa askari Magereza kutokulipwa kwa wakati na idadi kubwa ya wanaodai malimbikizo ya posho hizo.

**UHABA ASKARI**

Alisema Jeshi la Magereza linakabiliwa na uhaba wa askari wa kulinda wafungwa na kwamba kibali cha ajira walichopewa cha kuajiri askari 700 ni kidogo kulingana na uhitaji.

"Tunampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupa kibali cha kuajiri askari 700, lakini idadi hiyo ni ndogo kwa sababu tuna idadi kubwa ya maofisa ambao hawawezi kuwalinda wafungwa, wanahitajika askari wa vyeo vidogo kutekeleza jukumu hilo. Hivyo tunaomba askari wengi zaidi," alisema Mzee.

**UVAMIZI MAENEO**

Meja Jenerali Mzee alisema kumekuwapo na tabia ya uvamizi wa maeneo ya Jeshi la Magereza unaofanywa na baadhi ya viongozi wa serikali ambao wanawapatia wafanyabiashara.

Alisema tabia hiyo inasababisha Jeshi la Magereza kupoteza baadhi ya maeneo yake muhimu.

Kuhusu hospitali, Kamishna Jenerali Mzee alisema ilianza kufanya kazi mwaka 2017 kwa maofisa na askari wa Jeshi la Magereza kujitolea.

"Awali bajeti iliyopangwa kutumika kujenga hospitali hii ilikuwa ni Sh. bilioni 11, hadi sasa tumetumia Sh. bilioni 1.5, pia tumeamua kupunguza bajeti ya ujenzi hadi Shilingi bilioni sita hivyo tunahitaji Shilingi bilioni nne kukamilisha ujenzi. Tunakuomba utufikishie salamu zetu kwa Rais Samia atusaidie kumaliza ujenzi huu. Pia ikimpendeza pindi itakapokamilika jina la hospitali liitwe jina lake," alisema Kamishna Jenerali Mzee.

Kadhalika, alisema hospitali hiyo inatoa huduma zote muhimu ikiwamo uzazi wa mpango, kinamama, maabara, ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi na tiba za meno.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa miradi hiyo, Waziri Simbachawene alilitaka Jeshi la Magereza kuendelea kuibua, kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, pamoja na kuendelea kusimamia maono.

"Hili la madai ya posho nimelichukua na nakwenda kulifanyia kazi, Lazima nikaangalie tatizo lipo wapi, haiwezekani msilipwe posho zenu, kama tatizo lipo serikalini basi tutalitatua," alisema Simbachawene.

Kuhusu uvamizi wa maeneo, alilitaka jeshi hilo kuhakikisha linawatumia wataalamu wa masuala ya ardhi kuweka alama za mipaka katika maeneo yao yote.

Kuhusu mahabusi, Simbachawene alisema: "Hili suala ni zito kidogo kwa sababu lina mlolongo wa mamlaka. DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka) anahusika, Mahakama inahusika pia Jeshi la Polisi linahusika. Lakini tunakwenda kulifanyia kazi."

Miradi iliyozinduliwa ni nyumba za maofisa na askari Gereza la Wazo-Hill, mradi wa maduka ya kupangisha katika stendi ya mabasi Segerea, pamoja na uzinduzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi la Magereza Ukonga.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, akitumia kifaa kinachotumiwa na Idara ya Urasimu Ramani wakati wa mahafali ya Chuo cha Ardhi Tabora mwishoni mwa wiki. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Hatima sare JWTZ kesi ya kina Mbowe Januari

Na Mwandishi Wetu

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imepanga kutoa uamuzi mdogo katika kesi ya msingi Januari 10, mwakani, kwenye kesi ya Uhujumu Uchumi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Uamuzi huo unatokana na upande wa utetezi kuweka mapingamizi ya kutopokewa mahakamani kwa kielelezo namba 14 zikiwamo sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na ramani za vituo vya mafuta.

Vifaa hivyo vya kijeshi vinadaiwa kukutwa kwa mshtakiwa wa kwanza, Halfani Bwire, upande wa utetezi ukidai umekosa imani wa mnyororo wa kuhifadhi vielelezo hadi kufikishwa chumba cha mahakama.

Jaji Joachim Tiganga alitaja tarehe hiyo jana mahakamani huko mkoani Dar es Salaam baada ya upande wa mashtaka kumaliza kujibu hoja mbalimbali za mapingamizi zilizowasilishwa na upande wa utetezi kupinga kupokelewa kwa kielelezo hicho.

Mrakibu wa Polisi (SP), Jumanne Malangahe, ambaye ni shahidi wa nane wa upande wa mashtaka katika kesi hiyo, alioomba kutolewa kuwasilisha mahakamani vielelezo hivyo.

Hoja ya kupinga kupokewa kwa vielelezo hivyo iliibuka Ijumaa iliyopita baada ya mahakama kupokea kielelezo cha hati ya ukamataji mali ambapo hati hiyo awali ilipingwa kwamba ilikuwa na kurasa mbili na kwamba wakati anaanza kutoa ushahidi hakueleza kuwapo kwa kurasa mbili.

Wakili wa Utetezi, Nashon Nkungu, alidai shahidi huyo ambaye ni askari polisi hakuwahi kuieleza mahakama kuwa na utaalamu wa kuainisha sare za majeshi, zikiwamo alizodai ni za JWTZ na JKT alidai kumkuta nazo mshtakiwa Bwire.

Mbali na Mbowe na Bwire, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Adam Kasekwa na Mohamed Ling'wenya.

# JK aeleza umuhimu uhusiano kimataifa

Na Romana Mallya

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete, ameeleza umuhimu wa Tanzania kujenga uhusiano mzuri na mataifa mengine duniani ili kufanikiwa katika mipango yake mbalimbali ya kimaendeleo.

Kikwete aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika kongamano lijulikanalo 'Pamoja 60 Conference' lililoandaliwa na Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini nchini (REPOA) kwa ushirikiano na Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania.

Katika kongamano hilo ambalo liliangazia kutazama mafanikio ya ushirikiano wa Tanzania na Marekani kidiplomasia kwa miaka 60 iliyopita pia lilihudhuriwa na wanafunzi wa Chuo cha Diplomasia ambao walipata fursa ya kusikiliza viongozi mbalimbali waliokuwa wakihojiwa katika nyanja mbalimbali.

Kikwete alisema alipokuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Kimataifa, nia yake kubwa ilikuwa ni kujenga uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine duniani ili kulinda mipaka ya nchi dhidi ya matishio ya aina zote.

"Nia yangu ilikuwa ni kujenga uhusiano na mataifa mengine duniani ambayo niliyaendeleza hata nilipokuwa Rais kwa kuhakikisha tunakuwa na urafiki na dunia nzima na nchi jirani, SADC (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika), Bara la Afrika na kimataifa," alisema.

Pia alizungumzia sera ya mambo ya nje ambayo ililenga maslahi mapana ya taifa kwenye nyanja ya kimataifa katika diplomasia ya kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na kiusalama.

Alisema alipoteuliwa kuwa waziri wa mambo ya nje, alibaini mabalozi walihudhuria zaidi shughuli bila kufanya chochote cha kuisaidia nchi hivyo aliwasisitizia umuhimu katika diplomasia ya uchumi kwa kutafuta masoko, kukuza uwekezaji na misaada ya maendeleo.

Kikwete alizungumzia pia shambulio la bomu kwenye Ubalozi wa Marekani lililotokea mwaka 1998, ambapo alipigiwa simu na kuhusu tukio hilo, alijulishwa kuwa vyombo vya usalama vya Marekani vinasafiri kwa ndege kuja Tanzania na hakuna mtu anayepaswa kuokota chuma eneo la tukio.

Alisema alimpigia simu Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) wa wakati huo kumjulisha maagizo hayo kabla ya kupanda ndege kuelekea Zimbabwe ambako walikuwa wanakwenda na Rais Benjamin Mkapa, kuzungumzia matatizo kati ya Rwanda na Uganda.

Alisema pamoja na athari za shambulio hilo, lakini tukio hilo liliimarisha uhusiano wa karibu na ushirikiano kati ya vyombo vya usalama vya Tanzania na Marekani.

Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, alisema wamekutana hapo na viongozi mbalimbali kujadili hasa masuala yanayohusu diplomasia Tanzania na Marekani katika maeneo ya kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kiusalama.

Alisema miaka 60 imeleta manufaa kati ya nchi hizo mbili kwa kuimarisha usalama, uwekezaji katika eneo la miundombinu, afya, elimu na kufungua fursa za kibiashara.

HABARI KITAIFA

# Polisi ilivyoua watano wanaodhaniwa majambazi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WATU watano wanaosadikiwa kuwa ni majambazi wameuawa katika majibizano ya risasi na polisi mkoani Kigoma wakati walipokuwa wakitekeleza uhalifu wa kupora zana za uvuvi katika Ziwa Tanganyika.

Akithibitisha tukio hilo, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani humo, ACP James Manyama, alisema Desemba 19 majira ya saa tano usiku,

walipokea taarifa kutoka kwa waathirika waliokuwa wametekwa kisha kuanza ufuatiliaji na walipokaribia katika mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Tanzania waliwaona.

Alisema kulitokea majibizano ya kurushiana risasi kati ya polisi na watu hao na ndipo walipowapiga watu watatu ambao walijirusha kwenye maji na wengine wawili waliojeruhiwa walipelekwa Hospitali ya Rufani Kigoma Maweni ambako wakati wakipatiwa matibabu walipoteza maisha.

Jeshi hilo lilikamata baadhi ya mali zilizokuwa zimeporwa ikiwamo mitego ya samaki, injini tatu za mitumbwi na mafuta ya petroli.

Hamimu Lukoba, Mwenyekiti wa wamiliki wa vyombo vya uvuvi, alisema walipata taarifa mapema kuwa kuna majambazi watatekeleza tukio la uporaji na kuamua vyombo vyao vingi vya uvuvi kutovipeleka ziwani kwa kuhofia kuporwa.

Hata hivyo, alisema baadhi yao walifikiri habari hizo ni uvumi na kuamua kupeleka vyombo vyao ziwani.

Alisema wanalishukuru jeshi hilo kwa hatua za haraka za kupambana na majambazi hao kwa kuwa taarifa zilipopatikana utekelezaji ukaanza mara moja wa kupambana nao.

"Kwa kweli tunalishukuru jeshi letu kwa jitihada kubwa walizoonyesha, kama wataendelea hivi vitendo hivi vinavyotusumbua mara kwa mara vitakoma," alisema..

# DC mstaafu aondolewa mahakamani na polisi kukwepa waandishi habari

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Kitwala Komanya, anayekabiliwa na kesi ya madai ya fidia ya Sh. milioni 140 jana aliondolewa eneo la mahakama na askari wa Jeshi la Polisi akikwepa waandishi wa habari.

Baada ya mahakama kuahirisha shauri lake majira ya saa 03: 49 asubuhi, Komanya alishindwa kutoka nje kwa saa kadhaa akikwepa kupigwa picha na waandishi wa habari waliokuwa wakifuatilia mwenendo wa kesi yake.

Komanya alifika mahakamani hapo majira ya saa 02:56 asubuhi akiwa na gari aina ya DSUTA yenye namba za usajili T 500 DFY, alikaa ndani ya jengo hilo la mahakama hadi saa 12:42 mchana na kuondolewa na askari wa Jeshi la Polisi aliowaita kumtoa.

Mahakama ya Wilaya ya Tabora imeahirisha shauri lake hadi Desemba 27, 2021 ili lipangiwe hakimu wa kulisikiliza katika hatua ya usuluhishi.

Uamuzi huo umefikiwa na Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Tabora, Nzige Sigwa, baada ya kusilikiza maelezo ya makubaliano ya pande mbili kupitia kwa mawakili wao.

Shauri hilo inaonekana kuwa na mvuto wa aina yake kwa kuwa baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Tabora wakiongozwa na mbunge wa zamani wa jimbo hilo, Ismail Aden Rage, walifika kusikiliza hatima yake.

Mdai Ntonge kupitia kwa wakili wake, Kelvin Kayaga, aliiambia mahakama kuwa anatarajia kuleta mashahidi wasiopungua saba huku Komanya akiwakilishwa na Wakili Justine Sikon, akidai kuleta mashahidi sita wa utetezi.

Shauri hilo dhidi ya Komanya ambaye uteuzi wake ulikoma Juni 19, mwaka huu, baada ya kuenguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan limefunguliwa na Alex Ntonge mkazi wa mjini hapa.

Ntonge alifungua kesi hiyo ya madai akitaka alipwe Sh. milioni 140 kama fidia kutokana na vitendo vya udhalilishaji alivyofanyiwa na Komanya wakati akiwa Mkuu wa Wilaya.

Mdai katika shauri hilo kupitia kwa wakili Kayaga anadai alipwe kiasi hicho cha fedha kutokana na vitendo vya udhalilishaji alivyofanyiwa na Komanya Januari 5, 2021.

Ilidaiwa kuwa siku hiyo Komanya ambaye wakati huo alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Tabora akiwa ameambatana na askari wa Jeshi la Polisi walifika nyumbani kwake na kumdhalilisha.

Aliongeza kuwa walipofika nyumbani hapo walimkamata na kisha kumfanyia vitendo vinavyodhalilisha utu wake mbele ya familia yake na majirani zake

# Mamia wataabika usafiri, nauli zapanda

**Na Maulid Mmbaga**

WASAFIRI waendao mikoani hasa ya Kanda ya Kaskazini, wamejikuta kwenye wakati mgumu kutokana na magari mengi kujaa na wengine kulanguwa nauli.

Aidha, serikali imewataka wasafiri kutumia usafiri wa treni ambao ni wa uhakika na kuna nafasi za kutosha.

Nauli hizo zinadaiwa kupanda kwa magari binafsi ambayo husimama eneo la Mbezi Mwisho karibu na Kituo cha Mabasi cha Magufuli mkoani Dar es Salaam.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wasafiri waliokutwa kituoni wakitafuta usafiri, walisema magari mengi yamejaa hadi Desemba 24, mwaka huu, kiasi cha wengi kukosa magari huku nauli ikifika Sh. 50,000 kwa mtu mmoja.

Kwa mujibu wa nauli elekezi za LATRA Dar hadi Arusha basi la kawaida ni Sh. 22,700, daraja la kati 32,800 na daraja la kwanza 36,000.

Aidha, baadhi wamelalamika kutoa fedha zaidi ya kiwango kilichoandikwa kwenye tiketi na kujikuta wanatoa fedha nyingi na kukosa ushahidi.

"Nimekuja hapa tangu saa 12 alfajiri, jana walikataa kuniuzia tiketi wakasema nije leo asubuhi nimewahi ila sijui nitasafiri saa ngapi kwa kuwa kila basi ninaloenda wanasema wamejaza,"alisema Neema Massawe.

"Kinachofanyika wanakwambia nauli Sh. 50,000, lakini tiketi inaandikwa Sh.36,000 ukiwapa kiasi kilichoandikwa kwenye tiketi wanakunyima nafasi hadi uongeze fedha, wanapoteza ushahidi,"alisema.

Jana baadhi ya wasafiri waliokwenda eneo la Shekilango lenye ofisi nyingi za mabasi, lakini walisema hawakatishi tiketi za siku za mbele, bali abiria wanatakiwa kuwahi kwenye ofisi hizo ili wapate nafasi.

"Mama gari yetu imejaa hadi Desemba 24, ghairisha safari yako uende Desemba 25 au 26,"alisikika kondakta wa gari iendayo Ugweno, Mwanga mkoani Kilimanjaro akimweleza abiria.

MENEJA WA KITUO

Meneja wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Maira Chilosa, alisema huduma za usafiri zinaendelea vizuri na kwamba wapiga debe hawaruhusiwi kuingia ndani na kwamba hadi sasa hajapokea malalamiko ya kulanguliwa nauli.

"Katika kipindi cha sikukuu kiwango cha wasafiri hasa wanaoelekea mikoa ya kaskazini ni kikubwa, hivyo hakuna wapiga debe kwani magari mengi yanakuwa yameshajaa, na suala la uhaba wa usafiri wenzetu wa LATRA wameshakuja kuweka kambi kwa ajili ya kulishughulikia hilo," alisema Chilosa.

**KAULI YA LATRA**

Akizungumza na Nipashe jana Mkurugenzi LATRA, Gilliard Ngewe, alisema wamepiga kambi kituoni humo, ili kushughulikia suala hilo huku akidai magari yasiyo rasmi yanatoa huduma ya usafiri kinyemela kwani baadhi hayana vibali.

Aidha, alisema wameanza kutoa vibali kwa magari mengine yanayotaka kwenda mikoani hususani Kanda ya Kaskazini ili kuwasaidia wasafiri ambao ni wengi kwa sasa.

**USAFIRI WA TRENI**

"Watu wanalalamika shida ya usafiri, lakini ukiangalia usafiri wa treni upo na ina mabehewa 20 na hayajai, tangia Desemba Mosi, mwaka huu tulianza kutangaza ratiba kuwa itakuwa inasafiri Jumatatu, Jumatano na Ijumaa, lakini haijawahi kujaza, alifafanua na kuongeza;

"Watu wasifanye mambo kwa mazoea usafiri wa treni upo, lakini wanakubali kulanguliwa nauli. Nawasihi wasikubali kuibiwa."

Naye Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Wilbroad Mutafungwa, alisema wamejipanga kwa kipindi hiki cha mwisho wa mwaka kwa kuelimisha wasafiri na kuchukua hatua kwa madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani.

"Tunasisitiza madereva wa ujumla wasitumie vilevi wanapokuwa wanaendesha na endapo yoyote atabainika kukiuka agizo hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake, pia tunatahadharisha madereva wasiendesha kwa mwendo kasi ambao unaweza kuhatarisha usalama," alitahadharisha Mutafungwa.

Alisema kuna vizuizi kwa ajili ya kudhibiti madereva wanaovunja sheria na kwamba watakagua magari binafsi kujiridhisha kama wana vibali vya kubeba abiria na wanaosafirisha abiria usiku.

"Nitoe wito ni marufuku magari kusafirisha watu muda ambao hautambuliki kisheria, pia ni marufuku watu kupanda magari ya mizigo watumie magari halali, ambayo yamewekwa kwa kazi hiyo," alisisitiza Mutafungwa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI NA 2 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**YUDITHA STEVEN MSOFE.......MAREHEMU**
**MASALIA YAKOBO CHALE NA YOHANA MASALIA CHARLES.............WAOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwana haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa waombaji walioomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo kabla ya tarehe 30 mwezi desemba ,mwaka 2021

**Imewasilishwa mwanga leo tarehe 16,desemba 2021**

DISTRICT COURT MWANGA
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

**KUPOTEA KWA CHETI**



**NABARAKI L. MIBAROI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1442/0082 kilichotolewa Baraza na Mitihani la Taifa kupitia **MWANDET SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/MON/RB/381408/2021.**

RIPOTI MAALUM - 2

# Kitendawili cha usalama mahabusi walioko polisi

- Matukio yanavyokinzana na sheria za nchi
- Hospitalini kuna utata mpya unaojitegemea



**Na Waandishi Wetu**

**KATIKA sehemu ya kwanza jana, kulikuwa na simulizi yenye simanzi ya mama mfiwa wa mwana kutoka mkasa wa polisi, huku mzoefu wa kukaa mahabusu akianika mambo hasi aliyoyashuhudia mahali huko. Endelea kupata undani wa kinachojiri mahabusu hadi mamlaka ya juu kitaifa kukitolea angalizo:**

Ni takriban mwezi mmoja sasa tangu kuripotiwa kwa madai ya Issa Kassimu (22) kushambuliwa na askari polisi wa Kituo cha Polisi Goba wilayani Ubungo mkoani Dar es Salaam Novemba 10, mwaka huu, baada ya kukamatwa kwa tuhuma zinazohusiana na wizi.

Inadaiwa kipigo hicho kilisababisha alazwe kwenye chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICU) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Baada ya taarifa hiyo kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii na wanaodaiwa kuwa ndugu wa kijana huyo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alitoa taarifa kuhusu tukio hilo Novemba 16, mwaka huu, akisema hizo ni tuhuma nzito na wameshafungua jalada la uchunguzi.

Kamanda Muliro aliahidi sheria kuchukua mkondo wake kwa ajili ya hatua zaidi na kwamba tayari uchunguzi huo ulikuwa umeanza.

Vilevile, Septemba mwaka huu, baadhi ya askari polisi jijini Dodoma walidaiwa kufanya ukatili dhidi ya dereva wa pikipiki (bodaboda) kwa kumdhuru mwilini, ikiwamo sehemu za faragha.Iliripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwa dereva huyo mwenye umri wa miaka (21), mkazi wa jijini Dodoma, alilazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa kwa ajili ya matibabu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alithibitisha tukio hilo, lakini hakuwa na uhakika wa watu waliomdhuru kijana huyo na uchunguzi ulikuwa unaendelea.

Tukio lingine linaloshabihiana nalo ni la Mei mwaka huu wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro lililohusu tuhuma za polisi kuwajeruhi kwa kipigo wakazi wawili hadi kumvunja mmoja wao mikono kwa madai ya wizi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Amon Kakwale, alithibitisha kupata taarifa za tukio hilo lililokuwa tayari kwenye mikondo ya uchunguzi.

Pia kuna tukio la Desemba 21, mwaka jana, Stella Moses (30) alipodaiwa kujinyonga akiwa kwenye Kituo cha Polisi Mburahati wilayani Kinondoni.

Stella, mama wa watoto wawili, alidaiwa kujinyonga siku hiyo kwenye mahabusu ya polisi, huku ndugu wa marehemu wakitilia shaka taarifa hiyo ya polisi.

> Ni marufuku mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha." Katiba ya Tanzania, Ibara ya 13(6)(e)

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Ramadhan Kingai, alikaririwa akidai tukio hilo lilitokea Desemba 21, mwaka jana, leo ukiwa unatimu mwaka mmoja kamili tangu kuripotiwa kwa tukio hilo.

Hata hivyo, taarifa hiyo ya Kamanda Kingai inakinzana na ile ya ndugu wa marehemu waliodai ndugu yao alifariki dunia siku moja kabla, yaani Desemba 20 mwaka jana baada ya kujisalimisha katika kituo hicho cha polisi, alipopata taarifa kwamba alikuwa anatafutwa.

Wanandugu hao walilalamika kwamba hata walipofuatilia kituoni kwa ajili ya kumpatia chakula na mengineyo, walipewa taarifa tata kuhusu alikokuwa na hawakuwahi kumwona hadi taarifa ya umauti ilipowafikia.

**UZOEFU WA HOSPITALI**

Katibu wa Afya Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Rajabu Kaseke, alipofuatwa na Nipashe hospitalini huko, alikiri hupokea maiti kutoka Jeshi la Polisi pasipo kupewa ufafanuzi unaojitosheleza kuhusu vyanzo vya vifo vyao.

"Huwa inatokea mara kwa mara na leo (wiki mbili zilizopita) nimetoka kusaini vocha ya Sh. milioni 1.2 kwa ajili ya mazishi ya miili ya aina hiyo. Kwa hiyo inatokea. Hospitali hii ni kubwa na ni miongoni mwa hospitali zinazotegemewa katika kuhifadhi miili.

"Hapa ninaweza nisiwe na namba kamili ya idadi ya miili tunayoipokea kutoka polisi, lakini si kubwa sana na wala si ndogo sana. Inaweza kuwa miili miwili, mitatu kwa mwezi.

"Kwa hiyo, utaona ni hesabu kiasi gani kwa mwaka (24 hadi 36). Nikiongea na mtu wa mochwari au msimamizi wa kile kitengo, ninaweza kuwa na namba kamili. Tunashirikiana vizuri na Jeshi la Polisi, lakini niombe tu ushirikiano uzidi.

"Pamoja na kwamba tunaletewa mwili wa aliyekufa, basi wasiishie pale tu kutuletea mwili, bali tusaidiane zaidi kuwapata ndugu ili wachukue miili na kupunguza gharama kwa serikali," anashauri.

**ANGALIZO LA SHERIA**

Wakili Mpale Mpoki anasema ni kosa kisheria kwa askari polisi kumdhuru au kusababisha kifo kwa mtuhumiwa.

"Katiba ya nchi inasema kila mtu ana haki ya kuishi. Hata inapotokea kwamba mtu amehukumiwa kunyongwa hadi kufa, zipo taratibu za kufuatwa hadi kutekelezwa kwa adhabu hiyo," anasema.

Kwa kurejea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inatamkwa katika Ibara ya 14 kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.

Pia Ibara ya 13 na vipengele vyake kwenye katiba inapiga marufuku mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho alipokitenda hakikuwa kosa kisheria, hali kadhalika ikiainisha miongozo ya viwango vya adhabu kisheria kutozidi uhalisia.

Ibara yake ya 13(6)(d) ina ufafanuzi kuhusu haki za mahabusi aliye mikononi mwa chombo halali cha kisheria kwa ajili ya uchunguzi, ikitamka:

"Kwa ajili ya kuhifadhi haki ya usawa wa binadamu, heshima ya mtu itatunzwa katika shughuli zote zinazohusu upelelezi na uendeshaji wa mambo ya jinai na katika shughuli nyinginezo ambazo mtu anakuwa chini ya ulinzi bila uhuru au katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu."

Vilevile, kifungu chake cha 6(e) kinapiga marufuku mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha. Pia kuna masharti yamewekwa kisheria katika kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, yakisomeka:

"Pale mtu anapokufa akiwa mahabusu ya polisi au katika hospitali ya magonjwa ya akili, ukoma, makazi ya walemavu au gerezani, ofisa ambaye alikuwa amemweka mtu huyo kizuizini au aliyekuwa msimamizi wa sehemu hiyo, atatakiwa wakati huohuo atoe taarifa inayohusiana na kifo kwa karani wa mahakama mwenye mamlaka ya eneo ambapo mwili umekutwa na korona huyo au mtu aliyeruhusiwa. "Naye atatakiwa kuutazama mwili na kufanya uchunguzi kuhusiana na chanzo cha kifo kwa kuzingatia sheria yoyote itakayokuwa inatumika kwa wakati huo inayoshughulikia uchunguzi huo."

Vilevile, kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinatoa angalizo kwa mamlaka zilizomweka mtuhumiwa mahabusu ama kumfikisha mahakamani au kumtoa mahabusu ndani ya saa 24, isipokuwa kwa makosa yanayohusiana na adhabu ya kifo.

*Itaendelea kesho

HABARI KITAIFA

## Kichanga alivyookotwa jalalani

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MTOTO mchanga wa kiume anayekadiriwa kuwa na umri wa siku moja, ameokotwa akiwa hai katika dampo la takataka lililoko katika eneo la jengo la ghala la Chama cha Msingi (AMCOS) Chikukwe Kijiji cha Chikukwe Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara.

Inadaiwa mtoto huyo aliyekutwa amevilingwa kwenye kipande cha khanga alitupwa katika dampo na mtu asiyejulikana, huku ikidaiwa inawezekana kitendo hicho kilifanywa na mama yake mzazi baada ya kujifungua.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya asubuhi na kushuhudiwa na baadhi ya watu waliokuwa wakipita njia katika eneo hilo.

Lestisia Herman, alisema alipokuwa anapita alisikia sauti ya kitoto kichanga na aliposogea katika eneo hilo alikiona kikiwa kimelazwa kwenye gogo ambalo lilikuwa na pango.

Alisema baada ya kukiona kichanga hicho alikimbia mpaka ofisi ya serikali ya kijiji na kutoa taarifa ndipo serikali ya kijiji ilipofika sehemu ya eneo la tukio na kumchukua mtoto huyo.

Diwani wa Viti Maalum Kata ya Chikukwe, Joyce Piteje, alisema tukio hilo linasikitisha na kuongeza kuwa alishafika Hospitali ya Mkomaindo kumuona mtoto na kutoa vifaa mbalimbali vya kumsaidia yakiwamo maziwa ya kopo na nguo, huku akiwasihi wazazi waache vitendo vya kikatili dhidi ya watoto.

Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, Victoria Msala, alisema kitendo hicho ni cha kinyama na kuwataka wananchi hasa wanawake wanaopata ujauzito kulaani vikali vitendo kama hivyo na kueleza kuwa kama kuna tatizo lolote kati ya mke na mume, bora kuliweka wazi ili liweze kupatia ufumbuzi badala ya kumzaa mtoto na kumtupa.

Alisema walipata taarifa kutoka kwa wananchi juu ya kuonekana kwa kichanga hicho, hivyo kwenda katika eneo hilo na kumchukua na baadaye walimpeleka katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Masasi kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu.

"Kitendo hiki ni cha kinyama, kama serikali ya kijiji pamoja na mtaa tutashirikiana kuhakikisha tunamsaka mhusika katika kila kijiji ili achukuliwe hatua za kisheria. Hivyo tunawataka wananchi kutoa taarifa kwa mamlaka zinazohusika wanapobaini watu wanaohusika na vitendo hivyo," alisema Msala.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Masasi, Mkomaindo ambako kichanga hicho kimehifadhiwa, Grace Mnengela, alithibitisha kupokea kichanga huyo, na kwamba walimchunguza na kubaini kuwa hakuwa na tatizo lolote la kiafya, hivyo walimfanyia usafi na kumuhifadhi na anaendelea na afya nzuri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Mark Njela, alipotafutwa ila hakupatikana kutokana na simu yake ya kiganjani kuiita kwa muda mrefu bila majibu.

# Fatma Karume afunguka taarifa kurejeshewa uwakili

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASHERIA Fatma Karume amezungumzia taarifa za kupongezwa kwa kurejeshewa uwakili, akidai kuwa uongozi wa mahakama umekataa kumrejeshea leseni yake.

Katika ukurasa wake wa Twitter jana, Fatma aliandika kuwa, tangu mwisho wa wiki iliyopita alipata ujumbe mwingi wa hongera kwa kurejeshewa uwakili.

"Leo, gazeti moja limeandika nimerejeshewa uwakili huu si ukweli. Ukweli ni huu, majaji watatu wa Mahakama Kuu walibatilisha uamuzi wa Tume ya Nidhamu ya kunifuta uwakili, nikamwomba Msajili wa Mahakama Kuu kunirejeshea uwakili akakataa kwa sababu hizi mbili.

"Ya kwanza, uamuzi wa Elieza Fereshi (Jaji Kiongozi wakati huo) haujabatilishwa na lazima niombe kama mtu aliyetiwa hatiani. Mbili, serikali imekataa rufani ya uamuzi wa Tume ya Nidhamu. Msajili amekataa kunirejeshea uwakili kwa sababu hizi mbili. Barua yake ipo hapa." Aiweka katika ukurasa wake wa Twitter yake.

Fatma aliendelea kuandika kuwa, "Kwa hivyo eleweni hata Msajili wa Mahakama Kuu aheshimu uamuzi wa majaji watatu, huu utamaduni wa kudharau majaji upo mpaka mahakamani.

"Kwa hivyo eleweni viongozi wa mahakama wameamua hawataki kuheshimu uamuzi wa mahakama, hawataki kunirejeshea uwakili, uamuzi wa serikali wa kukata rufani, haubatilishi hukumu ya majaji watatu, lakini msajili kaamua yeye anaweza kudharau hukumu kwa sababu serikali imekata rufani.



Watu wakipata chini ya daraja la waenda kwa miguu jana, badala ya kutumia daraja ambalo limejengwa ili kuwarahisishia uvukaji wa Barabara ya Morogoro kwenda na kutoka Stendi ya Magufuli iliyoko Mbezi Luis Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Washikiliwa polisi madai kutaka kuchoma gari la mwekezaji

**Na Mohab Dominick,** NYANG'HWALE

JESHI la Polisi mkoani Geita linamshikilia mmiliki wa shamba, Gelvas Bambo na wenzake watatu kwa kosa la kufanya vurugu na kutaka kuchoma gari la mwekezaji wa Mgodi wa Mahagi, Mrisho Masebu.

Mgodi huo upo katika kijiji cha Izunya wilayani Nyang'hwale.

Eneo linalogombaniwa ni lenye uchimbaji wa madini ya dhahabu lenye urefu wa kati ya mita 50 kwa mita 30.

Akizungumza jana na gazeti hili kwa njia ya simu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuongeza kuwa lilitokea kwenye mkoa huo.

Kamanda Mwaibambe alisema hatua hiyo inatokana na mgogoro ulioko katika eneo la uchimbaji dhahabu kati ya wamiliki wa mashamba pande mbili baada ya mfumuko wa madini hayo.

"Mgogoro huo upo mahakamani, uamuzi wa mahakama ni kwamba shughuli za uchimbaji zisitishwe kwanza kwenye eneo hilo, lakini kwa pande hizo mbili mmoja ameshinda anapaswa apate mgawo wake na vurugu zimetokea wakati wa ugawaji wa mawe yanayosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu ndipo mzee Bambo hakukubali mawe yabebwe mpaka wote wamalize kesi," alisema Kamanda Mwaibambe na kuongeza:

"Ni kweli watu wanne tunawashikilia akiwamo Bambo kwa kufanya vurugu na kupelekea gari la mwekezaji kutaka kuchomwa moto na familia yake kwa lengo la kishinikiza mifuko ya mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu yasitolewe kwenye eneo lake mpaka mahakama itakapotoa idhini ya nani mshindi."

Naye mmiliki mwingine wa Shamba, Idrisa Hussein na wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo hilo walitumia fursa hiyo kumwomba Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Mbogwe, Mhandisi Joseph Kumburu, aruhusu kuendelea kwa shughuli za uchimbaji wa madini hayo kwa kuwa wachimbaji hawapo sehemu ya mgogoro.

Pia Idrisa alisema kuwa pamoja na kwamba shamba lake lilikuwa na mgogoro haukukwamisha shughuli za uchimbaji, hivyo anamwomba RMO huyo kuufungua mgodi huo uendelee kufanya kazi kwani madini ni mali ya serikali mtu mmoja asikwamishe.

Kwa upande wake kaimu mwenyekiti wa mgodi wa Mahagi Joseph Yabita akizungumza na waandishi wa habari mgodini hapo alikiri mgogoro huo kusababisha gari la mwekezaji anayesimamia leseni kutaka kuchomwa moto kwa mafuta ya petroli na mtoto wa Idrisa Bambo na kumwomba ofisa madini huyo kuwaruhusu waendelee na uchimbaji kwa kuwa wao si sehemu ya vurugu na kufungwa kwa mgodi huo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Kutegemea umeme wa maji hakutamaliza tatizo*

**JUZI** Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), lilifafanua kuwa nchi haina mgawo wa umeme na kwamba kukatika kwa nishati hiyo kunakojitokeza ni kwa sababu za nguzo au 'Transformer' kuharibika.

Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Maharage Chande, alisema hakuna mgawo wowote na hali imezidi kuimarika ikilinganishwa na mwezi uliopita baada ya mvua kuanza kunyesha kwenye baadhi ya maeneo nchini.

Alitolea mfano wa bwawa la kuzalishia umeme la Kidatu na Mtera ambako kiwango cha uzalishaji kinapaswa kuwa megawati 200 kilishuka kutokana na kupungua kwa maji, lakini kutokana na mvua sasa kinafikia 190 hadi 195 hali inayoridhisha.

Aidha, alisema Bwawa la Kihansi kiwango cha maji bado hakijaongezeka kutokana na kukosekana kwa mvua za kutosha mikoa ya Njombe na Iringa.

Ufafanuzi wa TANESCO ni mzuri, lakini bado hauakisi hali halisi kwenye majiji, miji na vijijini sio wa kuridhisha, kwa kuwa umeme unakatika mara kwa mara bila taarifa kiasi cha kusababisha majanga. Kuna wakati unaweza kufikiri kuna mtu anafanya kusudi kwa sababu unazimwa na kuwashwa mara kadhaa hali inayohatarisha vifaa vya umeme kuungua.

TANESCO inasema inatoa taarifa kwa umma inapotokea umeme kukatwa, lakini si wakati wote taarifa hutolewa, au inatolewa wakati tayari ukiwa umeshakatwa.

Watanzania wanashika kauli ya TANESCO sasa ni muhimu kuona uhalisia kwamba umeme haukatiki na kama ikitokea umekatika wananchi waelezwe tatizo, lakini isiwe ni kila wakati ni eneo hilo hilo jambo ambalo si sahihi. Tatizo la umeme limekuwa la miaka yote kwamba kila mwaka hasa wakati wa ukame hiyo inaonyesha kwa kiasi gani tunategemea umeme wa maji, lakini sasa kuna umuhimu wa kuangalia sera na sheria ili kuwekeza nguvu kwenye vyanzo mbadala.

Hali iko hivi katika wakati ambao bado gesi haijatumika vyema kuhakikisha inazalisha umeme wa kutosha, ni muhimu ukafanyika uwekezaji wa kutosha wa miundombinu na kudhibiti mianya yote ya upigaji. Mathalani, vipi viwanda vinataka kuzalisha umeme wake ni muhimu vikaruhusiwa kuliko kuvibana kununua kwa TANESCO pekee, pia nishati jadidifu wawekezaji waruhusiwe kuwekeza kwa wingi hasa kwa kuangalia vikwazo kwenye uwekezaji huo.

Kilio kikubwa kwa wawekezaji wa nishati jadidifu ni kuwapo masharti ya vibali zaidi ya 30, ambayo lazima mhusika ayafuate kwenye ofisi tofauti zilizoko mikoa tofauti, muda mwingi unapotea kwenye kufuatilia vibali.

Ni muhimu serikali ikawasikiliza wawekezaji hawa na kutatua kero ili kuongeza kasi ya uwekezaji kwenye sekta hiyo, kwa kuwa hakuna ubishi kuwa mwelekeo wa dunia ni kuwekeza kwenye nishati jadidifu.


Kuna chanzo kingine cha nishati jadidifu ni joto ardhi ambalo limegundulika lipo kwa wingi mikoa ya Songwe, Mbeya, Manyara na kwingine, utafiti umefanyika sasa ni kuvutia wawekezaji lakini kujifunza kwa wengine.

Kenya inazalisha umeme wa joto ardhi kwenye bonde la ufa ambalo limepita pia Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara nchini ambako kuna majimoto ambalo halijatumiwa vyema.

Kwa mujibu wa Wikipedia, inakadiriwa Bonde la Ufa linauwezo wa kuzalisha megawati 2000 iligundulika mwaka 1956 eneo la Olkariana uzalishaji ulianza mwaka 1981 zilizalishwa megawati 15 na sasa wanazalisha MW 256 na wanatarajia kufikia 576 ndani ya miaka 20 ijayo.

Jitihada ni kubwa na sasa utafiti umeshafanyika, lakini kasi iongezeke ili nchi iwe na vyanzo tofauti tofauti vya umeme kuondokana na kutegemea umeme wa maji pekee, ambao haijaonyesha mafanikio kwa miaka mingi hasa kipindi hiki cha mabadiliko ya tabia nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uhaba madarasa ubaki historia 2022

Na Sabato Kasika

**KWA** mara ya kwanza, wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022, wanatarajia kuanza masomo kwa pamoja, tofauti na miaka mingine ambayo walisoma kwa awamu.

Wanafunzi 907,802 wanatarajiwa kujiunga na shule mbalimbali za sekondari nchini mwaka ujao, bila kuwapo awamu ya pili au ya tatu kama ilivyokuwa ikifanyika miaka ya nyuma.

Hatua hiyo ya kutoanza masomo kwa pamoja, ilitokana na uhaba wa madarasa, ambao wanafunzi wengine kusubiri hata miezi miwili ili ujenzi wa madarasa ukamilike kwanza ndipo waripoti shuleni.

Yawezekana madhara ya mtindo wa wanafunzi wa kidato kimoja kutoanza masomo kwa pamoja yasionekane, lakini ninaamini kwamba, wakipishana muda wa kuanza masomo, baadhi yao watashindwa kufanya vizuri.

Ili kuhakikisha kwamba, wanafunzi wote waliochaguliwa kidato cha kwanza mwaka ujao wanaanza masomo kwa pamoja, serikali inasema inajenga madarasa manne katika kila ilipo shule ya sekondari ya umma nchi nzima.

Hiyo ni kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akisema tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma, wanafunzi wataanza masomo pamoja.

Akiwa katika mkutano mkuu maalumu wa uchaguzi viongozi wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) jijini Dodoma, Ummy anaweka wazi kuhusu utaratibu huo.

Ikumbukwe, mbali na kuanza kidato cha kwanza kwa mafungu, baadhi ya shule ziligeuza majengo ya maabara kuwa madarasa ya muda hali iliyoelezwa kuwa ilisababisha wanafunzi kutojifunza masomo ya sayansi kwa vitendo.

Njia hiyo ilitumika ili kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanaenda shule hata kwa awamu mbili au tatu, sababu kubwa ikiwa ni uhaba wa madarasa unaotokea kila mwaka wa masomo.

Pamoja na serikali kuamua kujenga madarasa manne kwa kila shule, ipo haja kushirikisha wadau wa elimu katika kufanikisha azma hiyo, lakini ujenzi huo uwe ni ajenda ya kudumu na endelevu, uhaba wa madarasa utabaki historia nchini, kwani hautakuwa wa kusubiri kusikia shule fulani ina uhaba ndipo mikakati ya ujenzi ianze.

Kwa mtazamo wangu ni kwamba, uhaba wa madarasa kila mwaka si jambo jema, hivyo ingefaa kila mmoja kwa nafasi yake akashiriki kikamilifu katika ujenzi huo ili hatimaye usiwepo uhaba wa madarasa tena nchini.

Iwapo ujenzi huo utakuwa ni ajenda ya kudumu kwa kushirikisha wadau wote wa elimu, kuanzia wazazi, kero itaisha, kwa kuzingatia kwamba, kila mwaka wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuongezeka.

Kwa mfano, wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021, walikuwa ni 759,706, lakini kwa wale waliochagulikuwa kujiunga kidato hicho kwa mwaka ujao ni 907,802.

Idadi hiyo ni kubwa kidogo kuliko ya mwaka 2021, hali ambayo ni wazi kwamba, kuna haja ya kujipanga zaidi hasa kwa kufanya ujenzi wa madarasa kuwa ajenda ya kudumu badala ya kusubiri kwanza matokeo.

Serikali imeamua kujenga madarasa manne kwa kila shule, ili kupunguza uhaba huo, lakini kuna haja ya kushirikisha wananchi katika ujenzi huo hasa kwa kuzingatia shule hizo ni zao.

Ninaamini kwamba, wazazi na walezi wakishirikishwa katika ujenzi huo wanaweza kutoa mchango wa hali na mali, kuanzia nguvukazi yao au fedha, kwa kuwa wao ni wadau wakubwa wa elimu.

Kimsingi, kushiriki katika shughuli za maendeleo ni jukumu la kila mmoja, kwa maana hiyo, wana mchango mkubwa katika ujenzi wa madarasa ili kuwapunguzia watoto wao kero za kila mwaka.

## FCC: Soko huria lisiwe kichaka bidhaa bandia

**Na Beatrice Shayo**

TUME ya Ushindani (FCC) imesema itaendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili kulinda ustawi wa biashara na usalama wa watumiaji wa bidhaa, ikionya kuwa soko huria lisiwe kichaka cha bidhaa bandia nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Urio, alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipofungua mafunzo ya wahariri wa habari za biashara kuhusu majukumu ya tume hiyo.

Alisema lengo kubwa la wafanyabiashara kupata faida kubwa ambayo huenda isipatikane kwa njia halali na wakati mwingine ama kupigana vita wenyewe au kuhujumiana. Urio alisema FCC inaendelea kutekeleza majukumu yake kuhakikisha hayo hayajitokezi na biashara kuendelea kushamiri nchini pasipo kuwapo na bidhaa bandia kwa watumiaji.

"Kama tunavyojua nchi yetu tangu miaka ya 1980 iliingia katika uchumi wa biashara huria. Tunaonya kwamba biashara huria isiwe na maana watu kufanya mambo kiholela, kufanya vurugu wao kwa wao, kuhujumiana na kuhakikisha wanapata faida kubwa kwa kumtesa mlaji," alisema Urio.

Mkurugenzi huyo alisema jukumu lao kubwa ni kuratibu na kuangalia shughuli hizo kwa ukaribu ili kuhakikisha chochote kinachofanywa hakikiuki misingi ya ushindani.

Alisema FCC imeandaa semina hiyo ili kuwajengea uwezo wahariri na kuwaongeza uweledi wao kwa habari za biashara ambazo tume imekuwa ikisimamia kwa ukaribu.

"Katika mkutano wetu wa leo (jana) tutawaeleza majukumu ya FCC na wenzangu wataeleza kwa kina shughuli zetu ambao kimsingi zinalenga kukuza na kulinda ushindani wa kibiashara nchini," alisema.

Urio alisema kuwa mbali na kukuza na kulinda shughuli za biashara nchini, pia wana jukumu la kumlinda mtumiaji wa bidhaa na huduma za biashara.

# Chongolo aitaka UWT ijiimarishe isiwe ombaomba

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameliagiza Baraza Kuu la Jumuiya ya Wanawake wa chama hicho (UWT) kujenga msingi wa kujitegemea na kuimarisha uchumi ili waepuke kuwa ombaomba.

Pia amewataka kutengeneza mfumo wa kuwa na wanajumuiya wanaojitambua ikiwamo wanachama ili waweze kuwa na jumuiya imara zitakazoleta maendeleo ndani ya jamii.

Chongolo aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa Baraza Kuu ambao utakuwa wa mwisho kwa mwaka huu uliofanyika jana jijini hapo.

Alisema UWT wanapaswa kuwa wabunifu katika miradi mbalimbali ambayo itainua uchumi wao kwa sababu wasipofanya hivyo watakuwa ombaomba na watu watawachoka.

"Naomba tekelezeni hilo kama ilani yetu inavyosema mkifanya hivyo basi mtakuwa na jumuiya imara inayoleta maendeleo kwa watu," alisema Chongolo.

Alifafanua kuwa kinachotakiwa ni vitu vyote viende sawa kwa sababu CCM ni imara na jumuiya zake nazo zinapaswa kuwa imara ili waweze kuongoza vizuri.

Kadhalika aliwataka kujenga mfumo imara ambao utawawezesha kuwa na wanachama bora ambao wataunda jumuiya bora yenye uhai.

Alisema wanatakiwa kuwa wanachama hai ambao wanajitambua kwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku ndani ya jumuiya.

Alisema kuna viongozi ndani ya mwaka mmoja wamepandishwa nyadhifa zaidi ya mara mbili au tatu kutokana na juhudi wanazofanya katika uongozi waliokabidhiwa.

Awali, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudensia Kabaka, alisema baraza hilo limetambua mikoa mitano iliyofanya vizuri katika usimamizi wa miradi iliyopo na kuanzisha miradi mipya katika mikoa yao.

Alisema, lengo la kufanya hivyo ni kuwatia hamasa viongozi wote katika mikoa ili wafanye kazi kwa weledi na ujasiri na hatimaye kuongeza mapato ya jumuiya hiyo.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni pamoja na Kusini Unguja, Mjini Unguja, Kaskazini Pemba, Geita na Tanga.

Alisema baraza hilo limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuongoza nchi huku akizingatia maslahi kwa wanawake.

"Katika hotuba zake Rais Samia anajipanga na kufanya utafiti, ni hotuba zenye upendo, lakini hivi karibuni tumeona akizindua kamati maalum ya kijinsia iliyolenga kukuza masuala ya kiuchumi kwa kinamama, Baraza linampongeza sana," alisema Kabaka..



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Lazaro Kilahala (kulia), akipokea baadhi ya nyaraka za makabidhiano kutoka kwa Monica Moshi ambaye alikuwa ameshikilia ofisi hiyo kwa muda. Makabidhiano hayo yamefanyika leo katika ofisi za makao makuu ya wakala huo zilizoko mjini Dodoma na kushuhudiwa na viongozi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambao walimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Mpango wa uwekezaji, utunzaji bima waanza

**Na Mwandishi Wetu**

MPANGO wa utunzaji, uwekezaji bima uitwao 'Fanaka Plan,' umezinduliwa, ambao utampa mteja faida mbalimbali.

Mpango huo ambao umezinduliwa kwa ushirikiano kati ya Jibilee life Insurance na Benki ya NMB,

licha ya kulinda maisha ya mteja aliyedhurika, pia unampa faida tele na uhuru wa kutunza fedha kwa utaratibu na muda atakaochagua.

Uzinduzi wa Fanaka Plan ulifanyika jijini Dar es Salaam jana, ambako Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi na Mkurugenzi Mkuu wa Jubilee Life Insurance, Karim Jamal, walitiliana saini na kuutaja mpango huo kuwa ni kwa Watanzania wote wenye akaunti NMB na wasio nazo.

Mponzi alisema Fanaka Plan ni mshirika sahihi wa watu wenye malengo ya muda mrefu na ya kati katika kujiimarisha kiuchumi na kufikia malengo binafsi, uwekezaji ukiwa ni wa kati ya miaka mitano hadi 20.

Fanaka Plan, ni uwekezaji ambao unakuwa na bima ya maisha kwa mteja. Hii inawawezesha Watanzania kuweka akiba kila mwezi katika vifurushi mbalimbali, ambavyo vinatoa faida kuanzia Sh. milioni 5 na kuendelea, huku mteja akitakiwa kuchagua kifurushi ama 'Plan' kulingana na uwezo wake wa kuchangia kila mwezi.

"Hii maana yake utakuwa unajiwekea akiba, pesa yako itakupa bonasi na ikitokea mteja akapata ulemavu wa kudumu kabla ya wakati aliopanga, NMB na Jubilee Life tutalipa mchango wa miezi 36, hata kama mteja alilipia miezi miwili tu na ikitokea akafariki, atalipwa bima kamili sawa na kifurushi alichochagua," alisisitiza Mponzi.

Alibainisha kuwa, licha ya faida hizo kwa watakaopata ulemavu wa kudumu ama kifo wakiwa kwenye Fanaka Plan, mteja atakayemaliza muda aliochagua bila kupata ulemavu ama kifo, atalipwa kifurushi chake chote na atakuwa na bima ya maisha hadi atakapofikisha umri wa miaka 90 bila kuchangia kiasi kingine.

Aliwataka Watanzania kufika kwenye matawi ya NMB kote nchini, ili waweze kupata maelekezo muhimu ya namna ya kujiunga na Fanaka Plan, ambao aliutaja kama mpango uliobeba suluhu za changamoto zitokanazo na ukosefu wa uhakika wa kipato, lakini ukijihakikishia mwekezaji mnyororo sahihi wa mtiririko wa fedha.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Jubilee Life, Karim Jamal, alisema wanajivunia aina ya ushirikiano uliozaa Fanaka Plan, ambao unazihusisha taasisi vinara, kampuni yake na NMB ambayo ni benki bora Tanzania.

"Tunaishukuru NMB kwa aina hii ya ushirikiano chanya unaowahakikishia wateja usalama wa fedha na maisha yao, ushirikiano uliobeba tija na matarajio ya kesho iliyo njema kwa watoto na familia ya mteja iwapo atapata ulemavu ama kifo wakati akiwa ameshaanza kuwa mwekezaji kupitia Fanaka Plan," alisema Jamal.

# Songea yafagiliwa miradi ya Uviko-19

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, David Silinde, ameipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa kukamilisha ujenzi wa miradi ya UVICO-19 na kuwataka wataalamu kuendelea kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kwa maslahi mapana ya Taifa.

Alibainisha hayo jana alipokuwa kwenye ziara ya siku moja katika Manispaa ya Songea kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19, ambapo katika ziara hiyo, aliambatana na Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, wataalamu pamoja na viongozi mbalimbali kutoka Manispaa ya Songea.

Silinde alisema kuwa lengo la kufanya ziara hiyo ni kufanya ukaguzi wa miradi ili kujiridhisha na kuhakiki fedha zilizotolewa na serikali kiasi cha shilingi milioni 660 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 29 kwa shule za sekondari na vituo shikizi ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea kama zimefanya kazi kama ilivyokusudiwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Aliongeza kuwa Sh. bilioni 304 zilitolewa kwenye halmashauri mbalimbali nchi nzima kwa lengo la kujenga miundombinu ya elimu ambazo zimeweza kujenga vyumba vya madarasa elfu kumi na tano (15000) tayari vimejengwa, madarasa ambayo yatasaidia kutatua changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari na vituo shikizi.

Alimpongeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea, Dk. Frederick Sagamiko, wakuu wa shule na kamati za ujenzi kwa usimamizi mzuri wa miradi ambayo ni mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambao umekamilika tayari kwa matumizi kwa asilimia 100 katika ubora uliotakiwa kama ilivyoagizwa na serikali.

Naye Dk. Frederick Sagamiko alisema kuwa miongoni mwa mikakati iliyosaidia kukamilisha utekelezaji wa miradi ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 kwa asilimia 100 ni kufanyika kwa mikutano ya utambulisho wa miradi kwa wananchi, kukutana na wakuu wa shule na kamati za ujenzi kwa lengo la kujadili namna ya kutekeleza mradi kwa wakati, kukutana na wafanyabiashara wauzaji wa vifaa vya ujenzi walioko Manispaa ya Songea.




Mwanzilishi na mlezi wa kituo cha elimu na malezi ya watoto cha Mwanangu Special Day Care & Camp; Rehabilitation Centre kilichoko Vikindu mkoani Pwani, Janet Manoni, akizungumza kwenye mkutano wa wazazi na wadau wa elimu maalum kituoni hapo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto 119 wabainika kifua kikuu

**Na Mwandishi Wetu,**
TABORA

SERIKALI imewataka wadau wa afya nchini kufuatilia familia zenye wagonjwa wa kifua kikuu ili kuokoa maisha ya watoto 119 chini ya miaka mitano waliobainika kuwa na ugonjwa huo baada ya kufanyiwa uchunguzi katika mikoa ya Singida na Tabora.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Riziki Kisonga, wakati akifunga shughuli za mradi wa CAP TB uliokuwa ukitekelezwa katika mikoa ya Tabora na Singida tangu mwaka 2017.

Alisema mradi huo umeibua wagonjwa wengi wa kifua kikuu chini ya miaka mitano jambo ambalo hapo awali lilikuwa linaondoa uhai wa watoto wengi bila kujulikana.

Dk. Kisonga alisema jitihada zinaendelea kufanywa na serikali kukabiliana na ugonjwa wa kifua kikuu uliokuwa chini ya mradi huo unaoratibiwa na Shirika lisilo la kiserikali la EGPAF.

Alisema mradi huo ulifanikiwa kuwafikia watoto 827,129 kwa uchunguzi wa kifua kikuu kutoka 335 mwaka 2017 hadi 1,852, mwaka huu.

Pia kuongeza idadi ya watoto walioanzishiwa matibabu ya kifua kikuu kutoka 303 hadi 1,851 kwa kipindi hicho.

Awali, Mkurugenzi wa Ufundi Shirika la EGPAF Tanzania, Dk. Chirspin Kimario, alimweleza Mkurugenzi wa Kinga nchini kwamba wanaishukuru serikali kwa jitihada za kufanikisha huduma za afya ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, kuweka mazingira wezeshi kwa wagonjwa wa kifua kikuu ili waweze kupata huduma bora za afya stahiki.

Pia walipongeza mpango wa taifa wa kifua kikuu na ukoma kwa kuwapa kipaumbele watoto katika mpango mkakati juu ya kifua kikuu.

Alisema mradi huo umetekelezwa katika halmashauri 12 za mikoa hiyo miwili na kufikia vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 45 ikiwamo 17 katika mkoa wa Tabora na 28 mkoani Singida.

Asilimia 91 ya watoto wanaopata huduma za afya chini ya mradi wa CAP TB umeokoa maisha yao.

## Vigogo h/shauri wanolewa bajeti ya mrengo wa kijinsia

**Na Yasmine Protace**

WAKUU wa idara mbalimbali katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Saalam, wamepatiwa mafunzo na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ya kuwajengea uwezo wa kuandaa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Ubungo, Beatrice Dominica, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

"Tumepatiwa mafunzo mazuri sana ya siku moja kutoka TGNP, mafunzo haya yatawajengea uelewa wa pamoja kwa wakuu wa idara kuandaa bajeti katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023," alisema.

Aliongeza kuwa TGNP Mtandao ipo ndani ya Manispaa ya Ubungo, hivyo wamekuwa wakifanya nao shughuli katika kusaidia jamii kwenye masuala ya jinsia na lishe.

Aliongeza kuwa, TGNP iko tayari kusaidiana na halmashauri yao katika masuala ya jinsia na lishe.

Alisema wamepata nafasi ya kuwaomba kuwasaidia katika masuala ya lishe, kwa kuwa Ubungo haijafanya vizuri.

"Ubungo hatujafanya vizuri katika lishe baadhi ya maeneo, hivyo tumepata nafasi ya kuiomba TGNP itusaidie, tutakaposaidiwa watoto wakipatiwa lishe bora watakuwa na afya bora, pia watakuwa wanafanya vizuri katika masomo yao," alisema Beatrice.

Alisema wanatarajia kuwasiliana na uongozi wa TGNP kwa ajili ya kuwaomba wawaandalie madiwani mafunzo jinsia.

Alisema pia katika kikao cha watendaji wa kata nao watapitishwa katika maandalizi ya bajeti, hivyo wameiomba TGNP ishirikiane na halmashauri hiyo ili watendaji wa kata waweze kupata elimu ya uelewa wa masuala ya jinsia na jinsi gani waingize katika mipango yao.

"Tupo katika kipindi cha maandalizi ya bajeti, nitawahimiza wakuu wa idara kuyaingiza yake yote tuliyoambiwa katika mafunzo," alisema Beatrice.

Aliongeza kuwa kabla ya kuwasilisha bajeti yao watawasiliana na TGNP ili waone masuala ya jinsia kama yapo vizuri katika bajeti .

Alitoa wito kwa taasisi ambazo zipo katika Manispaa ya Ubungo, kuwa kipindi cha kuandaa bajeti kuna mambo mengi ambayo serikali inafanya, hivyo wanaomba taasisi zingine zishirikiane nao katika kipindi cha maandalizi ya bajeti kuona zinafanyaje ikiwamo na watawasaidia kitu gani.

HABARI KITAIFA

# Mradi watoa mafunzo ya udhibiti sumukuvu

**Na Mwandishi Wetu, MANYARA**

SERIKALI kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeanza kutoa mafunzo kupitia Mradi wa Kitaifa wa Kudhibiti Sumukuvu.

Mafunzo hayo ya mradi wa Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination" yatakayotolewa katika wilaya 18 zilizoko mikoa 10 nchini.

Mafunzo ya mradi huo yalizinduliwa hivi karibuni wilayani Kiteto mkoani Manyara na kuhudhuriwa na washiriki 120, ambapo mradi huo upo chini ya Wizara ya Kilimo na TBS imekabidhiwa jukumu la kutoa mafunzo hayo.

Akizungumzia na waandishi wa habari wilayani hapa kuhusu wilaya na mikoa itakayonufaika na mafunzo hayo, Ofisa wa TBS, Jabir Abdi, alitaja wilaya hizo ni za Kondoa, Chemba, Bahi, Kongwa, Babati, na Kiteto.

Zingine ni Namtumbo, Newala, Nanyumbu, Nzega, Urambo, Kibondo, Kasulu, Buchosa, Bukombe, Itilima, Kilosa na Gairo. Kuhusu mikoa zilizoko wilaya hizo, Abdi alisema ni Dodoma, Manyara, Ruvuma, Mtwara, Tabora, Kigoma, Mwanza, Geita, Simiyu na Morogoro.

Aliwataja walengwa wa mafunzo hayo kuwa ni wafanyabiashara, wasafirishaji na wasindikaji wa mahindi na karanga pamoja na bidhaa zake.

Abdi alitaja faida za mafunzo kuwa yalenga kulinda afya za binadamu, kuwezesha biashara ya mazao ya mahindi na karanga, kulinda afya za mifugo na kuwezesha utoshelevu wa chakula salama.

Faida nyingine ni kuhimili ushindani katika masoko ya ndani, kikanda na nje ya nchi.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mbaraka Alhaji Batenga, alipongeza uamuzi wa serikali kuanzisha mafunzo hayo, kwa sababu chakula ni hitaji muhimu sana kwa binadamu na ustawi wa maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Hata hivyo, alisema usalama wa chakula unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa sumukuvu ambao husababisha madhara ya kiafya na hata kiuchumi.

Batenga, alisema sumukuvu huathiri zaidi mazao ya mahindi na karanga ambayo ni sehemu muhimu ya chakula cha Watanzania hapa nchini. "Kwa sababu hiyo sisi sote tunatakiwa kuzingatia mikakati ya kukabiliana na sumukuvu ili vyakula vyetu viendelee kuwa salama kwa muda wote," alisisitiza Batenga.

# Miundombinu chakavu ya treni yamsikitisha Waitara

**Na Neema Hussein,** KATAVI

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, amesikitishwa na miundombinu chakavu na huduma zinazotolewa kwenye kituo cha usafiri wa treni Mpanda mkoani Katavi.

Jambo jingine lililomsikitisha ni kukosekana kwa jengo la abiria tangu huduma ya usafiri wa treni uanzishwe miaka 50 iliyopita.

Waitara ameyasema hayo jana alipotembelea kituo hicho kuzungumza na watumishi pamoja na baadhi ya abiria, huku akimtaka Mtendaji Mkuu kutoa majibu ni lini jengo hilo litajengwa.

Alisema pia amepokea malalamiko kutoka kwa wananchi wanaoishi karibu na reli kutofahamu mipaka ya reli inapoishia jambo lililosababisha usumbufu pindi wanapofanya shughuli zao za kimaendeleo.

"Mimi nasema hili jambo halikubaliki na Rais, kazi hii hawezi kuipenda tukiacha iendelee kukaa hivi tutakuwa hatumsaidii hii imenipa picha kuwa kumbe hizi stesheni zote inabidi zikaguliwe inawezekana hali ni mbaya maeneo yote hata usafi tu jengo linanuka utafikili wanalala mbuzi hewa nzito sasa bajeti ya kusafisha tu hapo ni kiasi gani hicho?" Alihoji. Kwa upande wake Stesheni Masta wa Kituo cha Treni Mpanda, Emmanuel Mtawali, alisema mabehewa ni machache hasa ya kwenda Dar es Salaam, hivyo kupelekea abiria kulalamika kubanana ndani ya behewa moja pasipokuchukua tahadhari ya UVIKO-19.

"Hili tatizo litaboreshwa maana saizi tuna behewa tatu za kwenda Dar es Salaam kwa hiyo hata tukiongezewa mbili zikawa tano zinatosha sana, lakini kwa upande wa mabehewa ya mizigo hakuna tatizo," alisema Mtawali.

Baadhi ya abiria wanaotumia usafiri wa treni walisema kukosekana kwa jengo hilo ni usumbufu, na kwamba wanasimama muda mrefu, wananyeshewa na mvua wakiwa kwenye foleni ya kukata tiketi, wengine wanalala nje wakiwa na watoto wakati wa kusubiri treni.



Diwani wa Viti Maalumu (CCM), Kata ya Chikukwe Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Grace Chipiteje, akimuhifadhi kwenye kitanda maalumu katika Hospitali ya Mkomaindo mjini Masasi mtoto mchanga wa siku moja aliyeokotwa jana, baada ya kutupwa kwenye dampo la takataka kijiji cha Chikukwe na mtu asiyefahamika. **PICHA: HAMIS NASRI**

# 98 wapata huduma upasuaji mabusha

**Na Said Hamdani, LINDI**

WANAUME 98 wamepata huduma ya upasuaji wa mabusha, ngiri maji na henia chini ya mpango wa gharama nafuu ili kupunguza ukubwa wa tatizo hilo mkoani Lindi.

Daktari Kiongozi Idara ya Upasuaji katika Hospitali ya Sokoine, mkoani humo, Dk. Abdalla Chome, alisema hayo jana katika mahojiano na Nipashe.

Alisema mpango huo ni wa majaribio uliochukua kipindi cha wiki mbili, kuanzia Novemba 22 hadi Desemba 6, 2021 na ulihusisha wagonjwa wanaokabiliwa na ngiri maji na henia.

Dk. Chome alisema kutokana na ukubwa wa tatizo hilo mkoani humo, uongozi wa Hospitali ya Sokoine, uliamua kutafuta njia mbadala itakayosaidia kukabiliana nalo kwa kuweka kiwango kidogo cha gharama kwa mgonjwa mmoja kulipa Sh. 50,000 badala ya Sh. 200,000.

Alisema walipokea wagonjwa 124, lakini waliobainika kuwa na vigezo vya kupatiwa huduma ya upasuaji ni 98 wakiwamo ngiri maji na henia, operesheni 150 zikiwamo za ngiri maji 79 na henia 71, zimefanyika na kuleta mwanga mzuri wa matumaini kwa wahusika.

"Kukosekana kwa wafadhili wa kusaidia gharama za matibabu huku idadi ya waathirika ikizidi kuongezeka mkoani mwetu, tulikaa na kubuni njia ya kupambana nayo kwa kuwataka wagonjwa wachangie Sh. 50,000 kila mmoja," alisema Dk. Chome.

Alisema kiasi hicho cha fedha kilihusisha dawa na ununuzi wa vifaa tiba zikiwamo gloves za mikononi, wakati gharama za kitanda zikibebwa na hospitali husika ya Sokoine.

Vile vile, alisema uondoaji wa mabusha kwa wagonjwa wanaume 26 waliosalia na kuchukuliwa namba zao za simu na wengine watakaojitokeza, unatarajia kuanza tena kati ya mwezi Februari na Machi, mwaka kesho.

# Wilaya yaagizwa ujenzi wa madarasa usiku na mchana

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, ameuagiza uongozi wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma kuhakikisha wanaongeza kasi kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa

vikamilike kwa wakati kabla ya Desemba 25, mwezi huu na kukabidhi kwa mkuu wa mkoa ili vianze kutumiwa na wanafunzi wapya wa kidato cha kwanza mwakani.

Silinde alitoa agizo hilo akiwa ziarani mkoani Ruvuma akitembelea halmashauri sita za Madaba, Songea Manispaa, Songea Vijijini, Mbinga Vijijini, Mbinga Mji na Nyasa na kukuta halmashauri zingine tano zimekamilisha kwa asilimia mia kasoro Nyasa ambayo bado na kuwaagiza wafunge taa na kuanza kufanya kazi usiku na mchana kwani kazi zilizobakia si nyingi ni za ukamilishaji kama kupaka rangi, kuweka dali, na sakafu huku baadhi ya shule ambazo zipo mbali na mji wanaezeka mabati.

Aliongeza kuwa muda huu uliongezwa wa wiki mbili ulikuwa ni kwa ajili ya kukamilisha na kukabidhi majengo mapema na si wa kuanza kujenga, hivyo amewataka wakamilishe mapema ili kuwaruhusu wakuu wa shule na watumishi wengine waweze kwenda likizo ya sikukuu za mwisho wa mwaka ili kuwaepusha kufanya kazi wakati wa likizo kwa sababu madarasa hayo yote yanatakiwa Desemba 31 nwaka huu yawe yamekabidhiwa TAMISEMI kwa ajili ya kumpa Rais mama Samia Suluhu kama ahadi waliyompa wakati anawakabidhi fedha hizo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Kanali Laban Thomas, alimhakikishia Naibu Waziri Silinde kuwa mpaka Ijumaa madarasa yote waliyopewa watakuwa wamekabidhi kwa mkuu wa mkoa na wamepokea maelekezo yote aliyoyatoa na wataanza kufanya kazi mara moja likiwamo la kufanya kazi usiku na mchana kuharakisha ukamilishwaji wa vyumba vya madarasa na kwa kuzingatia ubora na thamani halisi.

Kanali Thomas alisema sababu kubwa iliyosababisha wao kuchelewa ni uhaba wa vifaa vya viwandani kama saruji na magari ya kusafirishia vifaa, ambayo wanakodi kutoka Wilaya ya Mbinga kuwa nashughuli zingine.



Kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami katika Kiwanja cha Ndege cha Musoma zikiendelea, mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aonya uharibifu mazingira chanzo cha maji Mbwinji - Masasi

**Na Mwandishi Wetu,** MASASI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amekerwa na vitendo vya uharibifu wa mazingira katika chanzo cha mradi mkubwa wa maji wa Mbwinji unaopeleka maji katika wilaya za Masasi na Nachingwea.

Dk. Jafo alionyesha hali hiyo wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua shughuli za uhifadhi na utunzaji wa mazingira wilayani Masasi mkoani Mtwara jana.

Alibaini kuwa chanzo hicho cha maji kinachopokea maji kutoka safu za milima ya Makonde kuna baadhi ya watu wanaofanya shughuli za uchimbaji wa madini, ukataji wa mkaa pamoja kilimo bila kibali.

"Kitendo chochote kinachohatarisha mazingira ya vyanzo vya maji hakikubaliki na tukifanya mchezo wananchi wa Masasi na Nachingwea watakosa maji.

"Na hatutakubali wananchi wetu wapate shida ya kukosa maji kwa sababu tu ya watu fulani. Sasa ninapiga marufuku kuanzia leo shughuli za ukataji mkaa, uchimbaji madini na kilimo," alisema.

Dk. Jafo alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kuanza mchakato rasmi wa kukitangaza chanzo hicho kuwa kinalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Aliongeza kuwa mara mchakato huo utakapokamilika, eneo hilo litatangazwa kuwa eneo maalumu lililolindwa na hakutaruhusiwa shughuli zozote za kibinadamu zinazohatarisha mazingira kwa lengo la kuhifadhi chanzo hicho cha maji ambacho ni muhimu kwa wananchi wa wilaya hizo mbili.

Waziri huyo pia aliziagiza kamati za usalama za wilaya za Masasi na Nachingwea pamoja na wilaya zingine zinazozunguka safu za milima ya Makonde kusimamia agizo hilo kwa maslahi ya taifa.

Mradi wa maji wa Masasi - Nachingwea ulitekelezwa mwaka 2012, ukigharimu zaidi ya Sh. bilioni 40 kwa lengo la kutoa huduma kwa wakazi zaidi ya 300,000 wa wilaya hizo mbili ambazo zilikuwa na kero kubwa ya maji kwa miaka mingi hadi pale serikali ilipoamua kuanzisha mradi huo mkubwa wa maji.

## Uwanja wa Musoma sasa kufungua anga

**Na Mwandishi Wetu**

IMEELEZWA kuwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma utakapokamilika utafungua usafiri wa anga kwa mkoa wa Mara na kuwa kiunganishi kikubwa na mikoa jirani ya Kanda ya Ziwa.

Hayo yamesemwa mkoani Mara na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, wakati akikagua ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilometa 1.75 ambapo utaruhusu ndege za Q400 Bombadier kutua kwa urahisi kiwanjani hapo.

Prof. Mbarawa alisema ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma unaogharimu kiasi cha shilingi bilioni 35.047 na mkandarasi anayetelekeza mradi huo ni Beijing Construction Company Limited ambapo kazi zinaendelea kwa kasi.

Kuhusu suala la fidia, Waziri Mbarawa alisema serikali imekwishalipa fidia kiasi cha shilingi bilioni 3.955 kwa wananchi waliopisha ujenzi huo.

Kaimu Meneja wa uwanja huo, Frank Msoffe, alisema kuwa ujenzi wa uwanja huo utakapokamilika utatoka katika daraja la 2C na kwenda 3C na kuruhusu kupokea ndege zenye uwezo wa kubeba abiria 70 hadi 80.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Mara, Mhandisi Vedastus Maribe, alieleza kuwa mradi huo unatarajiwa kukamilika Desemba 2022 na unahusisha barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya maegesho ya ndege, jengo la kuongezea ndege na jengo la Zimamoto.

## SBL sasa kuendeleza usakaji vipaji vijana

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) itaendeleza jitihada za kusaka vipaji vya vijana, baada ya kutangaza kukirudisha sokoni kinywaji chake cha Smirnoff Ice Black ambacho hakikuwapo sokoni kwa kipindi kirefu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Meneja uvumbuzi wa SBL, Bertha Vedastus, alisema kinywaji hicho sasa kitakuwa kinapatikana kila sehemu na kuwataka watumiaji wake kuendelea kukifurahia.

Bertha alisema pamoja na kuwaburudisha watumiaji wake, Smirnoff Ice Black imekuwa ikiunga mkono jitihada za kuendeleza vipaji mbalimbali vya vijana ikiwamo shindano la kusaka vipaji vya Ma-DJ wachanga ambapo tayari limeshafanyika mara tatu kipindi cha nyuma.

"Kikiwa pia ni kinywaji kinachounga mkono ukuzaji wa vipaji, baada ya kurudi sokoni tutakwenda mbali zaidi kwa kuunga mkono siyo tu kutafuta Ma-DJ bali hata vipaji vingine na kwa hiyo vijana wa Kitanzania waendelea kufuatilia kwa ukaribu ili waweze kusikia na kupata fursa kutoka Smirnoff Ice Black," alisema Bertha.

Smirnoff Ice Black, ni kinywaji kilichopo tayari kutumika klichochanganywa na Vodka na ambacho ni sehemu ya vinywaji vinavyozalishwa na kampuni mama ya SBL, Diage.

"Baada ya kusubiri kwa muda, sasa tumewaletea tena kinywaji hiki cha kimataifa ili muweze kuendelea kukifurahia. Ni kinywaji chenye ladha nzuri na ya kipekee ambayo unaweza kuifurahia na marafiki," alisema Bertha.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 21, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

**Vodacom inavyojitosa vifaa, elimu kuokoa watoto njiti**



Ukurasa 12

Mtizamo hasi hedhi kikwazo elimu kwa binti Tumbatu



Ukurasa 13

Serikali inavyopania kuokoa vijana

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Madereva wenyewe kuzikabili mimba za lifti kwa wanafunzi

• Ni wa daladala, bajaji na bodaboda

WANAFUNZI wa kike ni waathirika wa rushwa ya ngono inayotokana na lifti za madereva wa bodaboda na daladala, wanaowarubuni kwa chips, daftari, pesa za matumizi, maji na soda wakati wa jua kali.

Vyote vinapalilia kuleta uhusiano wa kimapenzi, ambao huwakwamisha mabinti hao kielimu.

Ili kukabiliana na tatizo hilo, kampeni ya 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' mkakati wa kuwanusuru wanafunzi mkoani Dar es Salaam imeshika kasi.

Ilianzia Ilala, Kinondoni na sasa imetua Temeke. Ni katika harakati za kupinga ukatili wa kijinsia, unaofanyika katika Siku 16 za Kukomesha Ukatili wa Kijinsia, kampeni zikianza kazi wilayani Temeke hivi karibuni.

Harakati hizo, zinakaribishwa na walimu, maofisa wa ustawi jamii na viongozi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Katika kampeni hiyo inayotoa elimu nyumba kwa nyumba, shuleni na vituo vya daladala, bodaboda na bajaj, huwahamasisha madereva na jamii kuacha kuwarubuni wasichana na kuwaacha wasome.

Madereva hao wanaodaiwa kuhusika na kuwaingiza wasichana kwenye rushwa ya ngono kwa lifti, wanaelimishwa kuwalinda na kuwasaidia kufika salama shuleni mapema na kurudi nyumbani pia.

Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), ndilo linalofanikisha kampeni hiyo kwa kushirikiana na kamati zilizoundwa na madereva hao, wanachama wa shirika hilo.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anasema elimu ya kupinga vitendo hivyo, inafanyika shuleni, nyumbani na vituo walipo madereva.

"Tunawafundisha kuacha kulaghai wasichana pia tunabandika stika kwenye vyombo hivyo zenye ujumbe wa Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi bila Rushwa ya Ngono Inawezekana".



Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za wilaya ya Temeke na wadau wengine wakiwa katika maandamano ya uzinduzi wa kampeni hiyo wilayani humo. **PICHA: SABATO KASIKA**

**JUKUMU LA KAMATI**

Janeth anasema, zipo kamati 72 zilizoundwa na madereva wa bodaboda, bajaj na daladala ambao idadi yao ni takribani 3,142 zilizoanzishwa wilayani Kinondoni na Ilala.

"Mbali na kutoa elimu madereva wanawafuatilia na kuwazuia wanafunzi kuzagaa vituoni, wanawatafutia usafiri wa haraka, ili wawahi shule au nyumbani wakisafirishwa na daladala," anasema Janeth.

Anayasema hayo anapozungumza kwenye uzinduzi wa kampeni hiyo wilayani Temeke na kufafanua kuwa njia hiyo inaokoa wanafunzi na mimba za lifti.

Janeth anasema WAJIK kwa kushirikiana na madereva wanawafundisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mbinu za kukwepa lifti za kuangamizwa.

"Ndilo jambo la msingi WAJIK tunalojivua kuona kuwa wanafunzi wameanza kujitambua siyo rahisi kurubuniwa kwa lifti," anasema.

WAJIKI inayowezeshwa na Taasisi ya Women Trust Fund Tanzania (WFT) inashirikiana na madereva hao, ambao ni kiungo muhimu kuondoa ngono kwenye vyombo vya usafiri, kwa mujibu wa maelezo yake.

"Tunaamini madereva na makondakta wakiamua kuacha kuhadaa wanafunzi ukatili huo wa kijinsia na unyanyasaji havitashamiri katika jamii yetu," anasema.

Anasema WAJIKI inatamani wanafunzi wasafiri salama na kutimiza malengo yao ya elimu na kuongeza kuwa ukatili wa ngono kwa wanafunzi ni miongoni mwa matukio yanayoendelea kuripotiwa nchini, wanayojitahidi kuyakabili.

Anaongeza kuwa, madereva hao kwa sasa wamebeba ajenda ya kupinga rushwa ya ngono na kuwalinda wanafunzi, kuendeleza mtandao unaotetea haki za wanawake katika kupinga ukatili wa jinsia.

Aidha, anataja malengo ya baadaye ya shirika hilo kuwa ni kutaka liwe na matawi kila mkoa, kwa kuwa vitendo hivyo havipo Dar es Salaam pekee, na kwamba linaendelea kujiimarisha ili kujitanua na kutimiza ndoto hiyo.

"Ukifuatilia historia yetu, utagundua kuwa tulianza kampeni mwaka 2018, lakini bado tupo maeneo machache kutokana na hali halisi ya kiuchumi, lakini ninaamini ipo siku tutafikia kile tunachohitaji kufanya," anasema.

"Takwimu za polisi, zinaonyesha

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA RAHMA SULEIMAN,
ZANZIBAR

# Mtizamo hasi hedhi kikwazo cha elimu kwa binti kisiwani Tumbatu

ZANZIBAR viko visiwa 63, kati yake saba vina wakazi na kimojawapo ni Tumbatu. Pamoja na kuwa ni visiwa, lakini huduma muhimu kama elimu hazikwepeki.

Kwa Tumbatu linapokuja suala la elimu kinamama na mabinti wa wanakabiliwa na changamoto zinazowarudisha nyuma, mfano kukosa taulo za kike wakati wa hedhi na mila za kuwafungia ndani kipindi hicho, yote yakiwarudisha nyuma kielimu.

Ni tatizo kwa wanafunzi na wanawake wa Tumbatu, mkoa wa Kaskazini Unguja kutokana na imani kuwa ukiwa katika siku zako huruhusiwi kutoka ndani.

Sheha wa Tumbatu Jongowe Miza Ali Sharif, anasema hedhi kwa wanafunzi wa kike ni moja ya changamoto zinazowakwamisha wanafunzi kimasomo.

Anafafanua kuwa baadhi ya wananchi wanaendeleza mila na desturi za kizamani zinazodai mwanamke au msichana anapokuwa na hedhi abaki ndani, hapaswi kushiriki shughuli za kijamii mfano kwenda shuleni.

"Zamani mwanamke au msichana unapokua katika siku huruhusiwi kutoka nje kwa imani kuwa anapotoka unaweza kupata madhara mfano kuvamiwa na mapepo," anasema Sheha Sharif.

Katibu Tawala wa Wilaya ndogo ya Tumbatu, Hatibu Habibu, anasema kisiwa kina wakazi 25,000 kati yao wanawake ni 13,000. Wanawake hao na wasichana wanatumia vitambaa vya asili wakati wanapoingia katika hedhi, na wasichana hulazimika kukosa masomo, anasema Kazija Shekha Pandu mwanafunzi wa kidato cha tatu Sekondari YA Tumbatu.



Kuhudhuria masomo, kucheza bila hofu wakati wa hedhi ni haki ya wanafunzi wasichana.
**PICHA: MTANDAO**

" Vitambaa tunavyotumia si madhubuti inatuwia vigumu kujisitiri hivyo hatuwezi kwenda shule wakati huo. Tunahofia mambo yanapoharibika inakuwa vigumu kukaa darasani kwenye mchanganyiko wa wanafunzi wa kike na kiume tunaamua kubaki nyumbani kwa siku kadhaa." Anasema Kazija.

"Sijawahi kutumia taulo za kike zaidi ya vitambaa vya asilia ambavyo wakati mwingine vinavuja. Lakini tunahitaji elimu ya matumizi ya taulo za kike za kisasa, lakini wanahitaji msaada wa taulo hizo kwa sababu wazazi na walezi wao hawana uwezo wa kuzinunua kila mwezi." Anasema.

Haroun Makame anayesoma kidato cha pili shuleni Tumbatu, anasema mara ya kwanza alipata elimu ya taulo za kisasa za kike baada ya Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation kufika shuleni kwao mwaka huu na kuwapatia msaada.

Anasema msaada huo uliwatatulia tatizo kwa muda, lakini saa zimemalizika kwa sababu walipewa za miezi mitatu na wameregea tena kwenye vitambaa.

"Shuleni pia hatuna maji ingawa vyoo vipo, vyoo bila ya maji ni sawa na mtoto bila wazazi au mzazi...ndiyo maana ninapokuwa katika hedhi nashindwa kwenda shuleni wiki nzima."

Sheha wa Tumbatu Jongowe Miza Ali Sharif, anasema hivi sasa mambo yamebadilika zamani mwanamke anapokuwa katika hedhi, hakuruhusiwa kutoka nje.

Leo taulo za kike za kisasa ni muhimu ni vyema taasisi mbalimbali na wadau wenye uwezo wasaidie kuwapatia msaada wasichana kwa sababu hali za kiuchumi za wananchi wa Tumbatu ni duni, anasema Sheha.

### UPATIKANAJI

Juhudi za kuwapatia wanafunzi huduma hiyo zinafanywa na hivi karibuni Sekondari ya Tumbatu ilipokea taulo 500 kutoka Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation, zilizokabidhiwa kwa Katibu Tawala wa Wilaya ndogo Tumbatu Khatib Habib Ali, anayesema mahitaji ya huduma hiyo ni muhimu kipindi chote ili wasome kwa furaha.

Anaeleza kuwa nia ya Serikali ya Zanzibar ni kuyapa makundi yote elimu ambayo ni haki ya msingi kwa mujibu wa katiba na hilo huhusisha wanawake.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo Asma Mwinyi, anawataka wanafunzi hao kuzitumia ili wasikose masomo na kwamba kukosekana taulo kunarudisha nyuma maendeleo ya elimu ya wasichana wakati wanafunzi wanaume wanasonga mbele.

Anasema mahitaji ya taulo hizo vijijini ni makubwa na elimu ya matumizi yake inahitajika ili wanafunzi kwa muda wote wahudhurie masomo.

Aidha, anazungumzia baadhi ya mila vijijini za kuwatenga wanawake wanapokuwa na hedhi na kutoshirikishwa katika huduma za kijamii, akisema ni masuala yasiyo na tija.

Anasema kwamba matarajio ya baadaye ya taasisi yake ni kufikisha huduma hizo katika kisiwa cha Pemba chenye visiwa vidogo vinavyoishi watu kukabiliana na changamoto kama hizo ambazo zinakwamisha wanafunzi.

Mkurugenzi wa kampuni ya Confidence Products Tanzania inayotengeneza taulo za kike, Fanta Kaijage, akizungumza kwenye hafla hiyo anasema wana mikakati kuhakikisha mtoto wa kike anakua salama muda wote na hedhi tena isimkwamishe kielimu.

''Tumekuwa tukitoa taulo mikoani ikiwamo Kagera, zimefika wilaya za Tunduma na Kigamboni na sasa tumefika Zanzibar kuwafikia watoto wa kike wenye mahitaji haya," anasema.

Mariyam Juma mwalimu wa Sekondari ya Tumbatu, anasema imani potofu kuwa msichana anapokuwa katika hedhi hapaswi kwenda shule kwa hofu ya kuchafua sare inaendelea na kwamba kwa kawaida darasa moja linakuwa na wanafunzi 45 na wakati mwengine wanafunzi wa kike zaidi ya watano hupata hedhi wakati mmoja na kusababisha upungufu na anapomuuliza binti kwanini hakuhudhuria shule anamwambia alikuwa katika hedhi.

Juma Mwadini Abdallah Ofisa Elimu Wilaya ya Kaskazini A Unguja, anasema taulo za kike ni hifadhi kwa wasichana ili kupata elimu akisema kinamama wana changamoto kubwa za elimu hivyo taulo hizo ni hitaji la msingi.

## Madereva wenyewe kuzikabili mimba za lifti kwa wanafunzi

**INATOKA UK.11**

matukio ya ukatili kwa watoto yanazidi kuongezeka, kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu yamefikia 6,168."

Kati yao wasichana ni 5,287 na wavulana ni 881, huku waliobakwa wakiwa 3,524 na waliolawitiwa ni 637, wavulana ni 567 na wasichana ni 70.

"Waliopata mimba ni 1,887 waliochomwa moto 130, wasichana 97 na wavulana 33, na watuhumiwa 3,800 wamekamatwa huku kesi 2,368 zikiwa zinafanyiwa uchunguzi, kesi 88 zimetolewa hukumu," anasema.

### VITA YA WOTE

Akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Temeke kuzindua 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', Ofisa Masoko wa wilaya, Doto Killangi, anawataka wananchi kushirikiana na wadau wote kukomesha ukatili wa kijinsia kwenye jamii.

Doto anasema, kila mtu anatakiwa kufanya sehemu yake kukomesha vitendo hivyo, ikiwamo kutoa za taarifa kwa vyombo vya dola, badala ya kuiachia serikali na asasi za kiraia zinazopambana na ukatili wa kijinsia.

"Ukatili wa kijinsia si jambo la kufumbia macho, kila mmoja afanye sehemu yake kukomesha vitendo hivyo, ili watoto wote na wanawake waweze kufikia ndoto zao," anasema Killangi kwa niaba na mkuu wa wilaya.

Anasema, kuna ukatili ni wa aina nyingi ukiwamo wa rushwa ya ngono ambao watoto wamekuwa wakifanyiwa katika jamii, na kwamba ni vyema jamii ikashiriki kikamilifu katika vita ya kukomesha vitendo hivyo.

Mwakilishi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wa wilaya hiyo, Esther Mkokota, anawataka madereva kutambua kuwa wana nafasi kubwa ya kusaidia wanafunzi kutimiza ndoto zao kwa kutowarubuni kwa usafiri.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Serikali inavyopania kuokoa vijana

BAADA ya taarifa kuwa idadi kubwa ya vijana wanaambukizwa VVU na kupata UKIMWI, hisia zinakuwa iwapo ndiyo waathirika wakubwa wa VVU, mbona sera, mipango na mikakati inajielekeza zaidi kwa watu wazima na watoto licha ya kwamba kundi hilo la rika balehe na wenye miaka chini ya 25 ndiyo wamaoumia zaidi? Desemba 1, siku ya UKIMWI Duniani, serikali ilitangaza kuwa maambukizi yamefikia asilimia 40 miongoni mwa vijana na kati ya hao asilimia 80 ni wasichana. Wanaoathirika wana miaka kati ya 15 na 25.

Ni kutokana na hali hiyo hiyo, Nipashe inazungumza na Desteria Nanyanga, Ofisa Programu Afya ya Uzazi kwa Vijana na Jinsia, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuelezea juhudi zipi zinazofanywa kisera, miongozo na mikakati ya kuwanusuru vijana na maambukizi mapya ya VVU.

Desteria anaanza kueleza mipango ya karibuni ya serikali kwenye kuwahudumia vijana yanapokuja masuala ya ngono na athari za kujamiiana bila kujitambua, akisisitiza kuwafunza elimu ya afya ya uzazi, kama anavyoeleza kwenye mahojiano haya...

**SWALI: Umezisikia takwimu, vijana hasa mabinti ni waathirika zaidi wa VVU, tuambie serikali inafanya nini ili elimu ya afya ya uzazi salama iwafikie vijana?**

**JIBU:** Imeanzisha Agenda ya Taifa ya Kuwekeza katika Maendeleo na Ustawi wa Vijana (NAIA) iliyozinduliwa Juni mwaka huu 2021 na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Agenda hii inalenga kutatua changamoto zinazowakabili vijana wenye umri wa miaka 10-19 kwa kuzingatia maeneo makuu sita muhimu kulinda na kuhakikisha ustawi wa vijana.

**SWALI: NI mambo gani?**

**JIBU:** Kuzuia mimba katika umri mdogo, pia kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI miongoni mwao. Kadhalika kuzia vitendo vya ukatili na uhalifu miongoni kwa vijana hawa. Aidha, kuboresha lishe shuleni ili kupunguza na kudhibiti utoro kwenye shule za msingi na sekondari ili kuwafanya wasichana na wavulana kubaki shuleni na kusoma.

Jukumu jingine tunalojipa kwenye mkakati huu wa NAIA ni kuwajengea uwezo vijana wetu kwenye stadi za maisha, kuwafundisha ufundi mbalimbali na elimu kwa vitendo.

**SWALI: Elimu ya afya ya uzazi salama ndiyo yenye 'nondo' za kukabiliana na maambukizi ya VVU, kuna miongozo yoyote iliyoandaliwa ili kufanikisha ufundishaji wake?**



Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, ofisi yake inaratibu ustawi na maendeleo ya vijana. **NA MPIGAPICHA WETU**

> **"Tunajengea uwezo watoa huduma ngazi ya jamii, wazazi, walezi na waelimishaji rika ili elimu ya afya ya uzazi kwa vijana ifikishwe kikamilifu kwenye jamii na kuwaunganisha vijana na vituo vya kutoa huduma za afya ili wavitumie na kunufaika.**

**JIBU:** Serikali inatengeneza na kufanya mapitio ya miongozo mbali ya watoa huduma kwa mfano, imeandaa mtaala wa kufundishia watoa huduma za afya ili waweze kutoa huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana kote nchini.

Inaangalia pia viwango vya utoaji huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana kulingana na mahitaji halisi.

Aidha, kuna mtaala wa kufundishia waelimishaji rika ili kutoa mafunzo yanayokidhi hali ya umri, uelewa na mazingira ya vijana wanaofundishwa.

Pamoja na hayo inafanya tathmini na ufuatiliaji shirikishi kwa watoa huduma kwenye vituo vya afya ili kufahamu uhalisia na manufaa ya kazi inayofanyika.

Pamoja na hayo inahakikisha uradibishaji masuala ya huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana kwenye kamati za afya za mikoa na wilaya ili masuala yao yafahamike na kufanyiwa kazi.

Pamoja na hayo tunawajengea uwezo wakufunzi na watoa huduma za afya ili waweze kutoa huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana na hadi sasa asilimia 39 ya watoa huduma za afya kote nchini wamejengewa uwezo.

"Tunajengea uwezo watoa huduma ngazi ya jamii, wazazi, walezi na waelimishaji rika ili elimu ya afya ya uzazi kwa vijana ifikishwe kikamilifu kwenye jamii na kuwaunganisha vijana na vituo vya kutoa huduma za afya ili wavitumie na kunufaika."

Juhudi zimefanywa kutengeneza mwongozo wa kutoa huduma za afya ya uzazi, masuala ya ukatili wa kijinsia na masuala ya UKIMWI kwenye vyuo vikuu na vyuo vya kati vyote hapa nchini ili kuhakikisha ustawi wa vijana.

**SWALI: hadi kufikia 2021 ni mwongozo upi unatumiwa na watoa huduma za afya katika kutoa huduma rafiki kwa vijana?**

**JIBU:** Pamoja na miongozo hiyo, Wizara ya Afya imeandaa viwango nane vinavyoainisha huduma bora na rafiki kwa vijana. Kiwango cha kwanza ni kamati za afya kuhakikisha vijana wanakua na uelewa wa afya zao, na kufahamu wapi na wakati gani huduma za afya ya uzazi kwa vijana zinatolewa.

Hapa kinacholengwa ni uongozi wa hospitali uweke mabango yanayoeleza kutolewa huduma rafiki kwa vijana na muda gani wanazipata.

Kiwango cha pili ni wazazi na walezi kuhakikisha vijana wanatumia huduma rafiki za afya kwa vijana. Aidha, vituo vya afya navyo vihakikishe wazazi na walezi wanapata uelewa mpana na umuhimu wa huduma rafiki kwa vijana kuhusu ujinsia na elimu ya uzazi salama.

Kiwango kingine ni huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana kutolewa kulingana na umri wa kijana na mahitaji. Kuwapo na watoa huduma wenye uwezo na weledi katika masuala ya afya ya uzazi kwa vijana ni kiwango kingine tunachotazama.

Mazingira rafiki yenye nafasi, yanayotengwa, saa maalam za kuhudumia vijana, uwepo wa dawa na vifaa tiba na huduma zinazotolewa kwa kuzingatia miongozo na sera ni kiwango tunachokisimamia.

"Kingine ni huduma kutolewa kwa usawa na bila kuwapo na unyanyapaa, wakati kiwango kingine kinachozingatiwa ni kutoa huduma kunakozingatia kukusanya, kuchakata na kutumia takwimu sahihi ili kuboresha huduma tunazotoa."

Kiwango cha nane ni kushirikisha vijana katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya huduma rafiki ya afya ya uzazi zinazotolewa na serikali kwa kundi hilo.

**SWALI: Unaweza kutaja mafanikio yaliyopatikana?**

**JIBU:** Ni pamoja na kuwapo kwa ajenda ya NAIA, sera na miongozo ikiwamo mipango ya kuwekeza kwenye maendeleo ya vijana na ustawi wao.

Kuhakikisha kuwa asilimia 63 ya vituo vya afya nchini vinatoa huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana haya pia ni mafanikio.

Halikadhalika asilimia 39 ya watoa huduma wanajengewa uwezo wa nanma ya kutoa huduma rafiki kwa vijana, huku elimu ikiwa imetolewa kwa wazazi na walezi kuhusu masuala ya afya ya uzazi kwa vijana yote ni mafanikio.

Pamoja na hayo serikali inaratibu wadau wanaotekeleza afua za afya ya uzazi hapa nchini kutoa huduma za elimu ya afya ya uzazi salama na ujinsia.

**SWALI: Unazungumziaje kuhusu changamoto?**

**JIBU:** Zipo baadhi ni kuwapo kiwango cha chini cha matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango miongoni mwa vijana. Nyingine ni mitizamo hasi ya watoa huduma kwa vijana, kukosekana usiri miongoni mwa watoa huduma wanaovujisha siri.

Tatizo jingine ni utoro shuleni, mila na desturi potofu na ongezeko la maambukizi VVU na UKIMWI miongoni mwa vijana wetu hasa wasichana na upungufu wa bajeti katika kutekeleza afua za vijana.

**SWALI: Nini ufumbuzi wa changamoto hizo?**

**JIBU:** Ni kutekeleza Agenda ya Taifa ya Kuwekeza katika Maendeleo na Ustawi wa Vijana (NAIA), tunapanga kuendelea kupunguza mimba katika umri mdogo.

Aidha, tutajitahidi kuendelea kuongeza vituo vya kutoa huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana kutoka asilimia 63 ya sasa hadi kufikia 80 mwaka 2025

Kadhalika tutaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma za afya kwenye masuala ya afya ya uzazi kwa vijana kote nchini.

Pia tumeazimia kuimarisha utekelezaji wa afua za afya ya uzazi kwa vijana shuleni, lakini tukiimarisha ushirikiano na sekta mbalimbali katika kutekeleza mpango wa NAIA, huku tukiimarisha na kuhamasisha elimu lishe shuleni na kuwapatia wanafunzi chakula kupunguza utoro.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Vodacom inavyojitosa vifaa, elimu kuokoa watoto njiti

Ni dua ya kila mwanamke anapobeba ujauzito kuomba kukutana na mwanawe aliyembeba, tena akitegemea kujifungua salama baada ya kutimiza miezi tisa.

Lakini, pamoja na matarajio hayo baadhi ya watoto wanaozaliwa hupoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kujifungua kabla ya kutimiza muda na kupata watoto njiti.

Chanzo cha watoto njiti kupoteza maisha kinaelezwa kuwa ni pamoja na kukosekana huduma muhimu za kiafya kama mashine za joto za kuwatunza maarufu kama 'incubators'

Taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kwamba duniani kote watoto njiti milioni 1.5 huzaliwa kila mwaka na kwamba na katika kila watoto 10 wanaozaliwa mmoja ni njiti.

Kutokana na changamoto hiyo Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, imekuwa ikitoa misaada mbalimbali ikiwamo 'incubators' kwa baadhi ya hospitali, zahanati na vituo vya huduma za afya kuokoa maisha ya watoto hao.

Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia, akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 67, anasema taasisi hiyo imekuwa ikitoa misaada katika eneo la afya ikiamini kuwa kukosekana vifaa tiba hivyo kunapelekea majanga kwa mama na watoto.

Roselyn anasema vifaa vya 'incubator' 'warm bed' ambacho ni kitanda maalumu kwa ajili ya kumsaidia mama wakati wa kujifungua na vingine vitakavyomsaidia anapopata uchungu pingamizi na vingine vya uchunguzi kama 'speculum' wameshavifikisha katika hospitali nyingi zilizoko Bara na Zanzibar ili kusaidia kina mama na watoto.

"Taarifa zinaeleza ni kwa namna gani kukosekana kwa hivi vifaa tiba kunapelekea majanga si tu kwa mama bali pia kwa watoto, njiti anapozaliwa hajakomaa kikamilifu hivyo wakati mwingine, mapafu yake hayajajijenga vizuri, anashindwa kuhema, kwa hiyo vifaa hivi vinaenda kumsaidia kuishi na kuimarika," anasema Roselyn.

Anasema taasisi hiyo ilianzishwa miaka 15 iliyopita, imekuwa ikifanya shughuli zake katika maeneo tofauti hapa nchini katika nyanja za elimu, mazingira, afya na kilimo ambapo kwa sasa wanamalizia harakati za kutumia mtandao wa simu kugusa eneo la kilimo.


Mtoto njiti akitunzwa ndani ya mashine ya kitabibu ya 'incubator'. **PICHA: MTANDAO**

> **Kuna tatizo la ajira ambalo wanataka sekta binafsi zifungue fursa nyingi ili kutoa ajira, kwani zipo ajira za moja kwa moja na ajira ambazo sio za moja kwa moja.**

Katika afya ya uzazi, mama na mtoto wamekuwapo kwa muda mrefu na kushiriki kampeni mbalimbali kama kutokomeza fistula wakishirikiana na Hospitali ya CCBRT, kwa kuwajengea jengo na kufanya kampeni za kuielimisha jamii uelewa kwa kutumia mtandao wa Vodacom, kutuma jumbe fupi (sms) na njia nyingine ili kupeleka habari za fistula.

"Tulitambua kuwa kuna kinamama wengi wanaishi na hii hali na hawapati tiba kwa sababu ya kukosa uelewa, tukasema kama watoa huduma ya mawasiliano tuna nafasi yetu ya kufanya na tulichokifanya katika eneo lile ni kutumia mawasiliano kutoa taarifa na kufanya kazi na watoa huduma za afya katika jamii kuwatambua kina mama hawa na kuwafikisha hospitali ambapo walipata matibabu bure," anasema Mworia.

Roselyn anasema baada ya kutekeleza mradi huo katika jiji la Dar es Salaam walifika Sengerema mkoani Mwanza mradi uliojulikana kama 'M-Mama' ambapo waligusia mradi huo wa afya ya mama na watoto kwa kushirikiana na serikali katika kutambua kinamama wenye shida ya uzazi ili waweze kupata matibabu ambapo waligusa maisha ya kinamama zaidi ya 4,500.

"Sasa tuko katika mazungumzo na Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI ili kuutekeleza mradi huo katika maeneo mengine kwa sababu tumeona kile kilichotendeka Sengerema kusaidia afya ya mama na watoto. Na katika maeneo ya uzazi tungependelea serikali kuweza kuupeleka mradi huu Tanzania nzima," anasema Roselyn.

Akizungumza wakati akipokea vifaa, Kaimu Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji wa Masasi, Dk. Amina Moshi, anapokabidhiwa vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi 67 milioni kutoka taasisi hiyo, anasema watoto njiti waliokuwa wakizaliwa kwenye halmashauri hiyo walilazimika kukaa wawili kwenye 'incubator' moja kutokana na uhaba wa kifaa hicho, hivyo baada ya kupewa nyingine itapunguza tatizo hilo.

Amina anasema halmashauri hiyo ilikuwa na changamoto ya vifaa tiba vingine kama 'warm bed' ambavyo huwasaidia watoto kupata joto mara baada ya mama kujifungua na oksijeni kwa watoto wanaokuwa na shida ya kupumua baada ya kuzaliwa.

Anasema halmashauri hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya vifo vya watoto wachanga ambapo Januari hadi Desemba 2020, kulikuwa na vifo vya watoto wachanga 165 na Januari hadi Julai 2021 kumekuwapo na vifo 63 hivyo kupatiwa vifaa hivyo kutapunguza changamoto hiyo.

Anasema kwa upande wa vifo vya kina mama Januari hadi Desemba 2020 vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 10, lakini Januari hadi Julai 2021 vilikuwa vifo sita hivyo, kupokea msaada wa vifaa vinavyosaidia kinamama wakati wa uzazi kutoka Taasisi ya Vodacom Tanzania ni hatua kubwa sana ya kusaidia kupunguza vifo hivyo.

"Tumepokea kitanda maalumu kwa ajili ya mama anayejifungua, vifaa maalumu vitakavyomsaidia anapopata uchungu pingamizi na vifaa vya uchunguzi kama 'speculum,' vyote kwa asilimia kubwa vitapunguza vifo vya mama na mtoto na kuimarisha huduma za afya wilayani hapa," anasema Amina.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Geofrey Mwambe, anazitaka taasisi za umma na wizara kuona zina wajibu wa kusaidia na kuhakikisha wawekezaji kwenye maeneo yao ili watengeneza faida kubwa na kutekeleza sera ya kurudisha kwa jamii.

"Ukiziwezesha taasisi au kampuni zikafanya biashara vizuri maana yake watapata faida kubwa zaidi na hivyo kutoa zaidi ya asilimia 30 ya faida ambayo itakwenda serikalini, hii itakuwa kubwa zaidi na hata ile asilimia kadhaa wanayotenga kupeleka kwa jamii itakuwa kubwa zaidi," anasema Mwambe.

Mwambe anasema kuna tatizo la ajira ambalo wanataka sekta binafsi zifungue fursa nyingi ili kutoa ajira, kwani zipo ajira za moja kwa moja na ajira ambazo sio za moja kwa moja.

"Vodacom wametengeneza fursa nyingi za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, kwa hiyo tuna jukumu kubwa kuhakikisha kampuni za namna hii zinakuwa nyingi si ili tu walipe kodi lakini pia waajiri watu na vijana wetu watapata mapato kuendesha maisha yao. Pia kwenye mapato ya mtu binafsi watalipa kodi mbalimbali, kwa hiyo vijana wengi wakiajiriwa tutapata fedha kodi nyingi kutoka kwa mtu mmoja mmoja," anasema Waziri Mwambe.



## HABARI DODOMA

# Ma-DC wapewa Desemba 28 kukamilisha ujenzi wa madarasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameagiza wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kuhakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kabla ya Desemba 28 bila kisingizio chochote uwe umekamilika.

Mtaka alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na wajumbe wa kikao cha kamati ya ushauri mkoa (RCC) kilichofanyika jijini hapa.

Alisema ni aibu kwa kiongozi aliyeteuliwa na Rais kushindwa kutekeleza jukumu hilo ndani ya wakati huku mikoa mingine wameweza.

"Lazima kama kiongozi wewe mwenyewe uwe na kiu ya kufanikisha jambo fulani haiwezakani leo eti kiongozi unasubiri kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa siku aliyopanga Waziri Ummy (Mwalimu) ya Desemba 31. "Hiyo ni siku ya waziri, lakini na wewe unatakiwa kuwa na tarehe yako kama leo unaulizwa wewe utakamilisha lini utajibu Desemba 31 kweli hapana, lazima viongozi tuwe na tamaduni zetu wenyewe lakini lazima tujifunze kwa wenzetu mbona Kigoma wenzetu wamemaliza na kukabidhi tayari," alisema Mtaka.

Katibu Tawala Msaidizi Serikali za Mitaa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Nathalis Linuma, alisema mkoa umepokea Sh. 16,164,937,108 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu kwa shule za msingi na sekondari.

Alisema miongoni mwa fedha hizo Sh.15,680,000,000 ni za Mpango wa Maendeleo ya Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

"Ambazo zinajenga madarasa kwa ajili ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2022 na Sh. 484,937,108 ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji na kuchimba visima," alisema.

Aidha, alisema ujenzi wa miundombinu hiyo katika halmashauri zote upo katika hatua mbalimbali na unapaswa kukamilika kabla ya mwezi huu kuisha.

Ofisa Elimu Taaluma Mkoa wa Dodoma, Abdallah Migila, alisema jumla ya wanafunzi 40,355 wamefaulu mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi na kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2022.

"Idadi hii ya wanafunzi ni ongezeko la wanafunzi 5,140 kulinganisha na idadi ya wanafunzi waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2020 ambapo wanafunzi 35,215 walifaulu,"alisema.

Kadhalika, alisema mkoa wa Dodoma umeendelea kuwatambua na kukusanya takwimu za wanafunzi walioacha shule kutokana na matatizo mbalimbali.

Alisema Mpango huo unafadhiliwa na mradi wa Sequip ambapo mpaka sasa wanafunzi 52, wamekubali na wapo tayari kuanza masomo nje ya mfumo rasmi Januari 2022.

Hata hivyo, alisema huduma ya chakula kwa baadhi ya shule za msingi na sekondari inatolewa kwa madarasa ya mtihani tu.

"Hivyo hakuna shule kwa mkoa wa Dodoma ambayo inatoa huduma ya chakula kwa madarasa yote kwa kipindi chote cha masomo," alisema.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Athony Mtaka, akizungumza na wafanyabiashara wadogo (machinga) wa Jiji la Dodoma (hawapo pichani) kwenye mkutano wa utiaji saini wa mkataba wa eneo litakalojengwa maalumu kwa ajili yao lililoko Bahi Road jijini humo, uliofanyika jana. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, Meya wa Jiji, Prof. David Mwafupe na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweli. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kiini cha migogoro ya ardhi chatajwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Enock Nyanda, amesema bado kuna vikwazo katika matumizi bora ya ardhi kwa jamii inayosababisha migogoro kila uchao.

Alibainisha hayo jijini hapa kwenye mkutano wa wadau wa mradi wa Ardhi Yetu unaoendeshwa na Shirika la Care International.

Alisema kwa sasa kumekuwa na tija kwenye sekta ya kilimo nchini huku kukiwa na vikwazo vya matumizi bora ya ardhi.

Nyanda alisema umuhimu wa utunzaji wa ardhi unatokana na matumizi ya ardhi kuongezeka na ukuaji wa kasi wa miji, hivyo kuifanya ardhi kupungua kila siku zinavyokwenda.

Alisema idadi ya Watanzania wanaoshiriki katika kilimo imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa tija katika sekta hiyo.

" Miaka ya nyuma wastani wa asilimia 70 ya nguvukazi ya Watanzania ilikuwa inajihusisha na shughuli za kilimo, lakini Sensa ya Kilimo,

Mifugo na Uvuvi iliyofanyika mwaka jana inaonyesha kuwa asilimia 58 ya Watanzania ndio wanaoshughulika na kilimo, jambo ambalo kinaonyesha umuhimu wa kuwa na mipango madhubuti ya matumizi endelevu ya ardhi.

"Ingawa idadi ya Watanzania wanaojihusisha kwenye kilimo kupungua, lakini upatikanaji wa chakula umeongezeka hali inayodhihirisha kuwa wakulima wengi wanalima kwa kutumia teknolojia zaidi."

Aliongeza: "Pamoja na tija kuongezeka lakini bado hatuna kilimo kinachohifadhi mazingira, bado tunachangamoto ya uhifadhi wa mazingira. Hapa tunatakiwa kwa pamoja kuwekeza nguvu zetu katika kukabiliana na hili."

# Waziri Jafo aziahidi ushirikiano NGO za mazingira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO) katika shughuli za uhifadhi wa mazingira.

Jafo alibainisha hayo alipokuwa akifungua kongamano la kukomboa ardhi iliyochakaa katika nyanda kame za Tanzania sambamba na maadhimisho ya miaka 10 ya shirika linalojihusisha na uhifadhi wa mazingira mkoani Dodoma la Lead Foundation.

Alisema kongamano hilo linatoa taswira ya namna gani NGO zinashiriki kikamilifu katika kusukuma mbele agenda ya mazingira nchini hivyo kuwajengea uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira.

"Niliwahi kuitisha mkutano na mashirika yanayojihusha na suala zima la mazingira na leo najisikia faraja kubwa kuona mashirika haya yanapiga hatua na lengo langu kubwa ni kuona kila mmoja anashiriki katika suala zima la uhifadhi wa mazingira," alisema.

Aidha, Waziri Jafo, alisema serikali itaendelea kusimamia Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira inayowashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wadau kutoka mashirika hayo.

Alisema anafarijika kutokana na Mpango Mkakati wa miaka 10 uliozinduliwa na Lead Foundation ambao unaonyesha namna gani shirika hilo linaunga mkono serikali katika hatua za kutunza na kuhifadhi mazingira husuan katika eneo la mabadiliko ya tabianchi linaloikabili dunia.

Aliwataka wananchi kutumia kipindi hiki cha masika kupanda miti kwa wingi na kuitunza ili kukabiliana na ukame ambao huleta athari mbalimbali za kijamii.

Aliwaelekeza wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia vizuri zoezi hilo na kuhakikisha misitu haichomwi ovyo ili kuepusha athari za mabadiliko ya tabianchi zinazochangia kukosekana kwa mvua.

Mwanzilishi wa Shirika la Lead Foundation, Askofu mstaafu Dk. Simon Chiwanga, alisema kazi ya ukumbozi wa mazingira inafanywa kwa namna mbili ambazo ni kuelimisha na kumbadilisha mtu fikra.



# Mifugo sasa kutambuliwa kielektroniki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imebuni njia mpya ya utambuzi wa mifugo bila kuharibu ngozi kwa kuweka heleni za kielektroniki masikioni ambazo zitasaidia kupata takwimu sahihi za mifugo nchini pamoja na kuainisha mahitaji ya wafugaji.

Zoezi la utambuzi wa mifugo kwa kupiga chapa ambalo serikali ilifanya nchi nzima mwaka 2017 linadaiwa kukumbwa na matatizo mengi ambayo yamesababisha zoezi hilo kutokuwa na ufanisi hali iliyoifanya serikali kubuni mbinu mpya.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mifugo kutoka katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Staford Barozi, alisema zoezi la awali lilikuwa linasababisha uharibifu wa ngozi za mifugo na hivyo kupunguza soko la bidhaa hiyo na kwamba zoezi hilo lilikuwa linakinzana na sheria.

Alisema kutokana na matatizo hayo serikali imeamua kuja na mfumo wa utambuzi wa mifugo kwa kutumia heleni za kielektroniki ambazo zina taarifa zote za mifugo ikiwamo taarifa za wilaya inakopatikana mifugo hiyo.

"Hizi heleni zina taarifa zote ambazo zinaweza kuingizwa kwenye mfumo kwa lengo la kutambua mifugo yote nchini, mfumo huu ni mzuri na una ufanisi mkubwa ambao utasaidia kuwa na takwimu zote muhimu za mifugo yote nchini," alisema Barozi.

Akizindua mafunzo kwa wataalamu mbalimbali watakaotekeleza zoezi hilo pamoja na wadau wa mifugo mkoani Mbeya, mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliwataka wataalamu hao kuutumia vizuri mfumo huo.

Alisema mfumo huo pamoja na kwamba ni mpya lakini sheria itakayotumika kwenye utekelezaji ni ile ile iliyotumika kwenye mfumo wa awali wa kupiga chapa mifugo ambao hata hivyo alisema haukuwa na mafanikio.

Alisema utambuzi huo wa mifugo kwa kutumia heleni hizo za kielektroniki utasaidia kuweka mipango mizuri ya mifugo ikiwamo upangaji wa matumizi bora ya ardhi.

Alisema mfumo huo utasaidia kujua idadi ya mifugo nchi nzima, mkoa na wilaya husika, kudhibiti wizi wa mifugo kutokana na kila mfugo kuwa na taarifa zake kwenye heleni hizo za kielektroniki na kuwezesha bima za mikopo kwa wafugaji.

"Mfumo huu pia utasaidia kukabiliana na magonjwa ya milipuko kwenye mifugo, kuwezesha serikali na wadau kuweka mipango ya kuboresha huduma za mifugo pamoja na kuwezesha mifugo iliyopotea kupatikana kwa kutumia taarifa za kielektroniki," alisema Mfune.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, aliiomba Wizara ya Mifugo na uvuvi kuboresha zaidi mfumo huo ili uwe na manufaa kwa wafugaji na taifa kwa ujumla ikiwamo kuwa na takwimu sahihi za mifugo.

Alisema mfumo huo unatakiwa kushirikisha mpaka ngazi za chini za serikali ambako ndiko kwenye idadi kubwa ya wafugaji na kwamba huko ndiko kunakuwa na ongezeko la mifugo.

Hata hivyo, baadhi ya wafugaji waliiomba serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuwashirikisha kwenye kila mfumo ili kuepuka kuwapo na taarifa za kuwachanganya.



Mwakilishi wa Shirika la SAWA linalotekeleza miradi ya ujenzi inayofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Joachim Asenga, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Shisyete katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya mwishoni mwa wiki kuhusu mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika Shule ya Msingi Shisyete. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Kijana mbaroni madai ya kujeruhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi linamshikilia kijana mmoja, Saimon Kabeta (23), mkazi wa Kijiji cha Lema wilayani Kyela kwa tuhuma za kumjeruhi Omary Kabeta (43) kwa kumtwanga na jiwe mguuni wakiwa kilabuni wanakunywa pombe za kienyeji.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 16, mwaka huu saa 8:00 usiku katika Kijiji cha Lema kilichoko katika Kata ya Usale wilayani Kyela.

Alisema mtuhumiwa alimjeruhi Kabeta na kumsababishia jeraha lililosababisha kuvuja damu nyingi, hivyo kukimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Kamanda Matei alisema chanzo halisi cha ugomvi wa watu hao hakijafahamika, lakini upelelezi unaendelea kufanyika ili mtuhumiwa apelekwe mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria na kwamba majeruhi anaendelea na matibabu.

"Hawa ni ndugu ni mtu na kaka, wameshambuliana wakati wanakunywa pombe kilabuni, lakini sisi kama Jeshi la Polisi lazima tuchukuwe hatua maana kushambulia mwenzio ni kinyume cha sheria za nchi," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi kwa madai kuwa ni kinyume na sheria hivyo akawataka kusuluhisha mambo yao kwa kuwatumia viongozi wa serikali.

Aliwataka pia wananchi kuacha kunywa pombe kupita kiasi kwa kuwa pombe ni chanzo cha matatizo mengi yanayotokea kwenye jamii ikiwamo kushambuliana.

Katika hatua nyingine, aliwataka wazazi na walezi kuwa makini na watoto wao katika kipindi hiki ambacho mvua imeanza kunyesha kwa madai kuwa kuna baadhi ya maeneo yanapita maji mengi ambayo yanaweza kuhatarisha maisha ya watoto.

Alisema watoto wadogo hawatakiwi kutumwa peke yao kwenda sehemu yoyote na badala yake waende na watu wazima kwa ajili ya ulinzi na usalama wao.

# Vijiji vyagombea umiliki wa zahanati Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa vijiji vya Maganjo na Itaga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameingia kwenye mgogoro wa kugombea umiliki wa Zahanati ya Maganjo ambapo kila upande unadai ndio wamiliki halali wa zahanati hiyo.

Wananchi hao wameiomba serikali kuingilia kati kumaliza mgogoro huo kwa madai kuwa umedumu kwa zaidi ya miaka 20 bila kupata suluhu na sasa unahatarisha amani baina ya wananchi wa vijiji hivyo viwili.

Wakizungumza wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, wananchi hao walisema mgogoro huo ulianza baada ya Kijiji cha Maganjo kugawanywa ambapo kila upande ulianza kudai kuwa zahanati ni mali yake.

Elizabeth Mwalindu, mkazi wa Maganjo, alisema zahanati hiyo ilijengwa na wananchi wa Igale kabla vijiji hivyo havijagawanywa lakini baada ya kugawanywa vijiji vya Maganjo na Itaga wakaanza kung'ang'ania.

Alisema kutokana na mgogoro huo wananchi hao wanapata shida kutokana na kukosekana mmiliki halali, hivyo akaiomba serikali iwasaidie kuumaliza kwa madai kuwa zahanati hiyo ni mali ya serikali kama ilivyo kwa taasisi zingine kama shule.

"Hapa tuna shida kubwa sana, hatuelewi kwanini mgogoro huu unaendelea, ilijengwa na watu wa Igale, lakini wanaogombana ni wa vijiji vingine ambavyo wakati huo vilikuwa kijiji kimoja tunaomba tusaidiwe," alisema Elizabeth.

Naye Edson Mwasembo, mkazi wa Kijiji cha Maganjo, alisema kwa sasa hawaelewi kama zahanati hiyo ipo kata gani kati ya Iwindi, Igale na Maganjo na hivyo akaiomba serikali kuwaainishia mipaka ya vijiji vyao.

Alisema mgogoro wa kugombea zahanati hiyo ulianza baada ya watu wasiojulikana kung'oa kibao kilichokuwa kinaitambulisha zahanati hiyo na kuondoka nacho.

Akizungumza baada ya kuwasikiliza wananchi hao, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, aliahidi kutuma wataalamu katika kata za Igale na Iwindi kuchunguza kiini cha mgogoro huo wa umiliki wa zahanati.

Aliwataka wananchi hao kuendelea na shughuli zao wakati wakisubiri majibu ya serikali yatakayotolewa baada ya timu ya wataalamu kumaliza kazi, na kwamba wanatakiwa waendelee kushirikiana kwenye mambo mbalimbali bila kubaguana.

Alisema wananchi hao watatakiwa kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa wataalamu hao kwa madai kuwa hao ndio watakaoainisha mipaka sahihi ya vijiji hivyo na kutoa majibu ya mmiliki halali wa zahanati hiyo ili kukomesha kabisa mgogoro.

"Wataalamu wetu wataonyesha mipaka na mipaka hiyo ndiyo itaonyesha nani ni mmiliki halali wa zahanati hii, kwa sasa naomba msibugudhiane bali mwendelee kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali," alisema Dk. Chuachua.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema kutokana na ongezeko la watu katika eneo hilo wanatakiwa kujengewa Kituo cha Afya badala ya zahanati na kwamba mgogoro huo hauna tija.

Alisema kikijengwa kituo hicho kitasaidia kuwahudumia wananchi wa kata tatu za Igale, Iwindi na Iyunga Mapinduzi ambazo zote hazina vituo vya afya.

## NMB yazindua kadi maalum kwa watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB imezindua biashara ya kadi ambayo itawezesha watalii kutohangaika wanapofanya manunuzi na malipo mbalimbali.

Uzinduzi huo uliofanyika hivi karibuni wakati wa mkutano wa mwaka wa Bodi ya Jumuiya ya Kampuni yanayotoa huduma ya Utalii Zanzibar (ZATO).

Akitoa ufafanuzi wa matumizi ya kadi hiyo, Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu NMB, Emmanuel Akonaay, alisema wamejipanga vyema kutoa suluhisho la huduma za kifedha, kwa kuwa na mifumo bora zaidi ya kubadilisha fedha, pamoja na biashara ya kadi ambayo itawezesha watalii kutohangaika wanapofanya manunuzi na malipo mbalimbali.

Alisema kwa kufanya biashara, kadi hiyo inaweza kufanya miamala yote ikiwamo kulipia kodi na malipo ya serikali, ushuru, tozo za utalii, ukusanyaji mapato ya ndani, ada za Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), TAMISEMI, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na ada ya paspoti ya kidijitali zote kupitia NMB mkononi. "Benki ya NMB ipo makini na uhitaji wa sekta ya utalii na wanaelewa wateja wanahitaji urahisi na ufanisi wa huduma za benki pamoja na suluhu mbalimbali endelevu za kibiashara," alisema. Alisema NMB imeweka kipaumbele kuhakikisha inasogeza huduma bora karibu na wateja, ili kuimarisha na kwenda na kasi ya uchumi wa buluu ambao kwa sasa ndio ngao ya uchumi huo.

"Tuna huduma ya ubadilishaji wa fedha za kigeni (Forex) pamoja na biashara ya kadi, pia tunalo jukwaa la biashara linalowezesha wafanyabiashara kufanya miamala kupitia tovuti zao (E-Commerce Platform), na tumewezesha matumizi ya kadi za malipo za 'UnionPay,'' aliongeza.

Pia alisema kadi hiyo inakubalika katika kufanyia miamala kwenye ATM na zile za kufanyia manunuzi (POS) za NMB, lengo likiwa kuleta huduma bora kwa wafanyabiashara kwenye sekta ya utalii. Aidha, alisema benki hiyo kwa kushirikiana na ZATO ilimeamua kuwarahishisha malipo na manunuzi ilikuleta manufaa, kwa kutumia kadi mpya ya malipo ya kabla (Prepaid Card) maalum kwa ajili ya wana ZATO.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, aliipongeza benki hiyo kwa kuzindua kadi hiyo, ambayo itarahisisha kufanya malipo ya aina mbali mbali pamoja na kuchangia pato la serikali kwa urahisi.

Alisema hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kufanya malipo yoyote ya serikali kuwa ya njia ya kielektroniki, hivyo mfumo huo utasaidia kuchangia pato la nchi kwa utalii ili kukusanya fedha nyingi.

Naye Mwenyekiti wa ZATO, Hassan Mzee, alipongeza benki hiyo kwa kuwa nao pamoja katika kuhakikisha biashara ya utalii inapiga hatua kubwa.

# Wasafirishaji watakiwa kuongeza safari za boti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, amewataka wamiliki wa vyombo vya usafiri Pemba na Unguja kuongeza ratiba za safari kutokana na kuongezeka kwa abiria kipindi cha Desemba na Januari.

Alisema hivi sasa watu wengi wamesafiri kwa mapumziko ya mwisho wa mwaka na sikukuu ya Krismasi na kwamba ni muhimu wamiliki wa meli na boti za abiria kuongeza safari kutokana na mahitaji.

Waziri huyo aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wamiliki wa vyombo ya abiria vya usafiri baharini katika ofisi za Mamlaka ya Usafiri Baharini, kutokana na kuongezeka kwa abiria wanaokwenda Pemba, Unguja na Dar es Salaam.

Aliwataka wamiliki hao pia kuangalia usalama wa abiria wakati wakiwa safarini.

"Hivi karibu nilifanya ziara kwenye meli zinazotoka Unguja kwenda Pemba nikakuta utiriri wa watoto huku wengine wakiwa hawana uwangalizi jambo hili ni hatari sana hasa ikitokea ajali pale," alisema waziri huyo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amour Hamil Bakari, aliwataka wamiliki wa vyombo hivyo kuchukua tahadhari ya UVIKO-19 kutokana na msongamano na kwamba kwenye ziara hiyo alibaini wengi hawakuwa na barakoa.

"Wiki iliyopita tulifanya ukaguzi wa abiria katika meli zinazofanya safari kati ya Unguja na Pemba hali ni ya kusikitisha hakuna aliyevaa barakoa wala kukaa umbali wa mita moja baina ya abiria na abiria,"alisema.

Aidha, aliwataka wamiliki hao kujitahidi kufuata taratibu na miongozo iliyopo na kuwasimamia mawakala wa uuzaji tiketi kwa kuwa kunasababisha usumbufu mkubwa.

Kuhusu idadi kubwa ya watoto wanaosafiri, wamiliki wa vyombo hivyo walisema licha ya sheria kutaka mtoto kuanzia miaka sita kulipiwa nauli lakini wazazi hawafanyi hivyo.

"Anakuja abiria akiwa ameongozana na watoto watano pengine wawili tu ndio wamekatiwa nusu tiketi. Hivyo ni muhimu kuwekewa kiwango maalum cha watoto kuwachukua katika boti wakiwa na tiketi,"alisema Mwakilishi wa Meli ya Flyinghose Nasrullah Morawey.

Aidha, wamiliki hao wameiomba serikali kuboresha miundombinu bora ya usafirishaji Bandari ya Malindi Unguja, ili kuondoa changamoto ya msongamano wa abiria na mizigo wakati wa kushusha na kupakia abiria bandarini hapo.

Meneja wa Kampuni ya Zan Fast Ferries, Rashid Aley, alieleza kuwa bandari hiyo ni ya muda mrefu tokea enzi za ukoloni na kwamba idadi ya watu ilikuwa ndogo, lakini hivi sasa matumizi ya bandari hiyo ni kubwa na miundombinu si rafiki.

Aidha, aliiomba Mamlaka ya Usafiri Baharini kutoa elimu kwa wananchi kuhusu usalama wa usafiri wa vyombo vya baharini wakati wanapokua safarini.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Ikraam Sealine co LTD ambayo inajishughulisha na usafiri wa abiria baharini, Abdulghafour Ismail (kulia), akizungumza katika kikao cha wamiliki wa usafiri baharini na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu usalama wa usafiri, kilichofanyika Malindi Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yatafuta fedha kukarabati mahakama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inatafuta fedha kwa washirika wa maendeleo au mkopo kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa majengo ya mahakama ambayo baadhi ni chakavu.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora), Haroun Ali Suleiman, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Bumbwini Mtumwa Peya, aliyetaka kujua lini jengo la Mahakama ya Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja litafanyiwa ukarabati mkubwa.

Waziri huyo alisema ni kweli jengo la Mahakama ya Mkokotoni pamoja na mengine yapo kwenye hali mbaya ya uchakavu kwa sababu yamejengwa muda mrefu sasa.

Alisema kwa muda mrefu serikali imeweka nguvu zake katika mradi mkubwa wa ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu huko Tunguu Wilaya ya Kati Unguja ambapo ujenzi wake upo katika hatua za mwisho kukamilika.

Alisema serikali imewekeza nguvu kwenye ujenzi wa mahakama mbalimbali zilizoko wilaya za Unguja na Pemba.

Alisema yapo majengo mengine ya mahakama yalioko Konde, Micheweni Pemba yanahitaji ukarabati mkubwa ili kuyawezesha kuendesha hukumu mbalimbali.

"Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23 tunakusudia kutekeleza mradi wa ukarabati mkubwa wa majengo ya Mahakama yalioko Unguja na Pemba ili kuyawezesha kuwa na hadhi ya hali ya juu...tunatarajia kutekeleza mradi huo katika hatua mbalimbali kwa kuwashirikisha washiriki wa maendeleo au mkopo," alisema.

Aidha, alisema ni muhimu kuwapo kwa majengo bora ya kisasa ya mahakama ambayo yatatoa nafasi nzuri ya usikilizaji wa kesi za wananchi kwa faraha zaidi.

Alisema zipo baadhi ya mahakama zilioko vijijini zinakabiliwa na uhaba wa nafasi za kusikiliza mashauri ya wananchi katika mwenendo wa kesi zinazowakabili kiasi cha kushindwa kupata nafasi nzuri.

# MISA-TAN yawanoa waandishi sheria za habari

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

TAASISI ya vyombo vya habari kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA-TAN), imetoa mafunzo kwa wanahabari mkoani Shinyanga, juu ya sheria ambazo zinagusa tasnia ya habari ili kuwaongezea weledi katika taaluma yao na kuepuka kuingia kwenye adhabu za ukiukwaji wa sheria hizo.

Kaimu Mkurugenzi wa MISA-TAN, Andrew Marawiti, akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, alisema waandishi wa habari wanapaswa kuzijua sheria na kuziishi ambazo zinagusa tasnia yao, pamoja na kuzipigia kelele zile ambazo zinaminya uhuru wa habari.

Alisema, taasisi hiyo imekuwa ikiendesha mradi wa miaka miwili wa utoaji wa elimu za sheria za habari kwa wanahabari nchini, kwa kushirikiana wa Taasisi ya International Media Support (IMS), ili kuongeza uelewa wa kuzifahamu sheria hizo na upungufu uliopo, ambao unapaswa kufanyiwa maboresho ili kutoa uhuru wa habari.

"Sheria ambazo zinagusa tasnia ya habari ni ya huduma za habari (2016), Takwimu (2019), na Sheria ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta (EPOCA) 2010," alisema Marawiti.

Kwa upande wake mwezeshaji wa mafunzo hayo, Jesse Kwayu ambaye ni Mhariri Mwandamizi kutoka Kampuni ya Media Brain, alisema waandishi wa habari wanapaswa kuwa makini na sheria ambazo zinagusa tasnia hiyo, kwa sababu baadhi ya vifungu vinawabana katika utekelezaji wa majukumu yao na kunyimwa uhuru wa kupata au kutoa taarifa.

Aidha, alisema serikali inapaswa kuzifanyiwa marekebisho sheria ambazo zinagusa tasnia hiyo kwa kurekebisha baadhi ya vifungu ambavyo vina minya uhuru wa habari, ili ziwe rafiki kwa ustawi wa nchi.

Nao baadhi ya waandishi wa habari, walisema elimu hiyo ya sheria zinazogusa tasnia ya habari, zitawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao na kuepuka kuingia kwenye matatizo.



Makamu wa Rais wa GGML anayeshughulikia miradi endelevu, Simon Shayo (kulia), akipokea tuzo kutoka kwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Being'i Issa (katikati). Tuzo hiyo imetolewa kwa GGML kwa kutambua mchango wa kampuni hiyo katika kutekeleza vema mwongozo wa maudhui ya ndani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEEC yaitunuku GGML tuzo ya mwekezaji bora

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limeitunuku Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) tuzo maalumu ya mwekezaji bora anayeshirikisha kikamilifu Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji kwa mwaka 2021.

GGML ilikabidhiwa tuzo hiyo jijini Dar es Salaam katika kongamano la tatu lililoandaliwa na baraza hilo na kufanyika kwa siku mbili.

Akikabidhi tuzo hiyo kwa Makamu wa Rais wa GGML anayesimamia miradi endelevu, Simon Shayo, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Being'i Issa, alisema GGML ni kampuni iliyotekeleza vyema mwongozo wa Local Content na kuwa chachu kwa wadau wengine katika kuwezesha ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji nchini.

Aidha, akifafanua sababu za kuipatia GGML tuzo hiyo, Katibu huyo wa NEEC alisema kampuni imeajiri wafanyakazi wengi zaidi ya 5,000 ambao ni Watanzania lakini vilevile katika menejimenti ya kampuni hiyo zaidi ya asilimia 90 ya viongozi wake ni wazawa.

"Pia imekuwa ikitekeleza programu ya kuwajengea uwezo wananchi wa Geita wanaozunguka mgodi ili waweze kushiriki kazi katika mgodi huo.

"Kwenye mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR), kampuni ya GGML pia inaongoza kufanya vizuri tofauti na kampuni nyingine katika sekta ya madini.

"GGML pia inatekeleza programu nyingine ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa Geita ili waweze kupata zabuni ndani ya kampuni hiyo na kampuni nyingine. Hayo ni baadhi ya mambo ambayo yametufanya tuone ni vema kuwatambua GGML," alisema.

Alisema mbali na tuzo hiyo ya mwekezaji bora ambayo GGML ilipata, pia kuna tuzo ya kampuni bora ya kitanzania na tuzo ya wasimamizi bora wa miradi ambazo zote huandaliwa na NEEC na kutolewa kila mwaka.

Aidha, alisema lengo la kuipatia GGML tuzo hiyo pamoja na washindi wengine ni kuhamasisha kampuni zingine ziweze kuiga mfano wa GGML.

"Kwa sababu pamoja na kuwekeza, tunachoangalia ni uwekezaji wenye faida ndani ya jamii na taifa kwa ujumla. Pia tuzo zinalenga kuleta ushindani ili watu wafahamu kwamba ni jambo la muhimu kwa kampuni hizi kuunga mkono juhudi za serikali kuwaletea maendeleo wananchi wake.

"Lakini serikali inaweza kutambua katika hilo eneo kwa sababu ukiangalia kwa mfano, GGML wanatoa fedha kwa Halmashauri za Geita zaidi ya bilioni 10 kila mwaka ambazo zinasaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii, hivyo ni vyema kuwatambua," amesema.

Hata hivyo, alisema kongamano hilo linapanua ukuaji wa uchumi wa nchi ya Tanzania pamoja na kupanua wigo wa ajira kwa Watanzania pamoja na kupunguza umaskini wa kipato.

"Local content' imelenga kuzalisha ajira kwa wingi hususani kwa vijana ambapo ajira 52,000 zimeshazalishwa nchini kutokana na programu ya 'local content' ambapo asilimia 70 ni vijana kati ya umri wa miaka 20 mpaka 35," alisema.

## 'Wenye ulemavu wapelekwe shule'

**Na Sabato Kasika**

WAZAZI wametakiwa kutowaficha watoto wenye ulemavu kwa kuwapeleka shule ili wapate elimu ambayo itawasaidia kuwajengea uwezo wa kumudu maisha yao ya baadaye.

Wito huo ulitolewa jana na mwanzilishi na mlezi wa Kituo cha Elimu na Malezi ya watoto cha Mwanangu Special Day Care &Camp; Rehabilitation Centre kilichoko Vikindu mkoani Pwani, Janeth Manoni.

Mwanzilishi huyo alikuwa akizungumza katika mkutano wa wazazi na wadau waliokutana kujadili yaliyojili mwaka huu na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto kwa mwaka ujao, 2022.

Janet alikuwa akijibu hoja mbalimblai zilizoibuliwa na wazazi kuwa watoto wao wananyanyapaliwa katika shule nyingi na hata zile zinazowakubali, hazina miundombinu rafiki kwa watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

"Wazazi acheni mtindo wa kufungia watoto ndani, kuwaficha na kuwatenga na wenzao, kwa kuwa kufanya hivyo kunawanyima haki zao za msingi na pia ni kuvunja haki za watoto na haki za binadamu kwa ujumla," alisema Manoni.

Alitaka vikwazo visiwakatishe tamaa, kwa kuwa serikali inasisitiza kutokuwapo na kikwazo chochote katika upatikanaji wa elimu kwa watoto wote na kuwataka wawapaleke shule.

"Tunayo mifano halisi kwa watoto walio hapa mbele yetu ambao waliletwa kituoni kwa mara ya kwanza hawakuweza kujimudu kwa lolote, lakini ndani ya mwaka mmoja, mnaona maendeleo yao," alisema.

Alisema, wanaweza kufanya mambo yao binafsi ikiwamo usafi, michezo na pia darasani wamepiga hatua kubwa, huku akitaka ushirikiano ili kuibua watoto wengine zaidi walio mitaani ili nao wapate elimu.

Kwa upande wake, Sukaina Esmail, Makamu wa Rais wa Club ya Lion tawi la Uhuru Dar es Salaam, akikabidhi vifaa mbalimbali vilivyotolewa na taasisi yake, alipongeza juhudi zinazofanywa na kituo hicho kuwapa elimu watoto hasa wenye ulemavu.

Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na magodoro, mashuka, vyandarua, mito, maziwa, sukari, vitakasa mikono, dawa za meno, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya msimu wa masomo kwa mwaka 2022.

"Tunatambua changamoto zilizoko katika kulea mtoto mwenye ulemavu. Wapo wazazi wanaokata tamaa kwa sababu ya umaskini au vikwazo vinavyosababishwa na jamii tunamoishi hivyo uwapo wa shule kama hizi ni mkombozi sio tu kwa mzazi bali pia hata taifa kwani kila mtoto ana haki ya kupata elimu," alisema Sukaina.

## Maelfu waandamanaji waandamana Sudan

**Khartoum,** SUDAN

MAELFU ya waandamanaji wamejitokeza jijini Khartoum, kuendelea kuwapo madarakani serikali ya kiraia, baada ya jeshi kuchukua madaraka nchini humo.

Maofisa wa usalama walitumia mabomu ya machozi, juzi, kuwasambaratisha waandamanaji ambao kwa mwaka wa tatu baada ya kumwondoa kiongozi wa zamani Omar Al Bashir, wameendeleza maandamano.

Maofisa wa usalama walitumia mabomu ya machozi kuwasambaratisha waandamanaji, waliokuwa wamefika mbele ya Ikulu ya rais.

"Huu ni uthibitisho kuwa watu wa Sudan ni imara. Tunaweza kuuangusha uongozi huu kama tulivyofanya kwa ule uliopita. Ni uthibitisho kuwa mateso hayaturudishi nyuma.

"Lazima maamuzi ya wananchi yaheshimiwe, hatutakubali kuongozwa na mtu ambaye aheshimu uamuzi wa watu," alisema mmoja wa waandamanaji.

Waliojeruhiwa walikimbizwa hospitalini kwa kutumia pikipiki, huku waandamanaji wakisema hawahofu lolote na wataendelea na maandamano kushinikiza kupatikana kwa serikali ya kiraia.

**RFI**

## Rais Ramaphosa arejea ofisini

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS Cyril Ramaphosa amerejea ofisini kwake, baada ya kumaliza wiki mbili za kujitenga kutokana na kupata maambukizi ya virusi vya corona.

Taarifa kutoka Ikulu ya rais ilisema hayo jana.

Ramaphosa, amechanjwa chanjo dhidi ya Covid-19, Johnson & Johnson, Februari mwaka huu, alipata maambukizi ya virusi hivyo wiki iliyopita.

Rais huyo anatarajia kuongoza kikao cha Baraza la Mawaziri siku ya kesho, taarifa ya Ikulu ilisema.

Siku chache zilizopita taifa hilo lilihusishwa na taarifa za kirusi kipya omicron, na kuathiri watu 20,000 kwa siku, ingawa takwimu hizo zilishuka mwishoni mwa wiki.

**REUTERS**

## Hukumu ya Suu Kyi Desemba 27

**Naypyidow,** MYANAMAR

MAHAKAMA nchini Myanamar ambako jeshi ndilo linaloshikilia madaraka imeahirisha kutoa hukumu jana katika kesi ya kiongozi aliyepinduliwa madarakani, Aung San Suu Kyi.

Duru ilileza kwamba, mahakama hiyo imesogeza mbele hadi Desemba 27, mwaka huu, kesi hiyo.

Mahakama ilitarajiwa jana kutoa uamuzi kuhusu kesi ya umiliki wa simu za upepo bila kibali pamoja na teknolojia ya kuzuia mawasiliano.

Makosa ambayo kwa pamoja yanaadhabu kali ya hadi miaka minne jela.

Jaji aliyetarajiwa kutoa hukumu hakutoa sababu za kuahirishwa kwa hatua hiyo.

**DW**

# Safari za ndege Nairobi, Dubai zasitishwa

**Nairobi,** KENYA

SAFARI za ndege zenye usafiri wa abiria kuingia na kupitia Dubai kutoka Kenya, zimesitishwa kwa muda wa saa 48 kuanzia jana.

Agizo kutoka kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Dubai, wateja hawatakubaliwa kusafiri kwa ndege za Emirates jijini Nairobi wakati huu. Hakuna sababu maalum iliyotolewa.

Katika taarifa kwenye tovuti, Emirates ilisema shughuli za abiria kutoka Dubai hadi Nairobi, hazijaathiriwa.

"Wateja walioathirika hawahitaji kutupigia simu mara moja ili kusajili upya nafasi tena. Wateja wanaweza kushikilia tikiti yao ya Emirates na safari za ndege zikirejea, wawasiliane na wakala wao wa usafiri au ofisi, kuweka nafasi ili kupanga mipango mipya ya usafiri."

Mei, mwaka huu, Kenya ilikataa ombi la Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) la kuongeza safari za ndege kutoka Dubai hadi Nairobi na Nairobi hadi Dubai.

Katika hatua inayoonekana kulinda Shirika la Ndege la Kenya Airways, Waziri wa Uchukuzi wa nchi hiyo, James Macharia, alisema serikali imeazimia kunyima ndege za Emirates ruhusa ya kusafiri kati ya miji hiyo bila vikwazo.

Emirates ilifanya safari 14 kwa wiki kutoka Dubai hadi Nairobi na kurejea tena Nairobi hadi Dubai.

Waziri huyo alisema uamuzi wake ulilenga kulinda maslahi ya taifa, ikizingatiwa kuwa mkataba wa sasa wa huduma za anga kati ya nchi hizo mbili, ulikuwa wa upande mmoja na unaopendelea Emirates.

**BBC**




Wakazi wa Jiji la Chicago nchini Marekani wakiwa eneo la Millennium Park, kufurahia sikukuu za mwisho wa mwaka, Krismasi na Mwaka Mpya. **PICHA: XINHUA**

## Jeshi la Ethiopia laudhibiti mji wa Lalibela

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

VIKOSI vya Ethiopia, vimechukua tena udhibiti wa mji wa Lalibela, huku Kiongozi wa Jimbo la Tigray, akizilaumu Uturuki, Iran na Falme za Kiarabu (U.A.E), kuchochea mgogoro nchini Ethiopia.

Shirika la habari la Ethiopia, limeonyesha picha za Naibu Waziri Mkuu akitembelea mji wa Lalibela.

Hata hivyo, haijafahamika ni lini vikosi vya serikali vilichukua udhibiti wa mji huo, ulio na umuhimu mkubwa kwa Wakristo wa madhehebu ya Orthodox.

Wapiganaji wa kundi la ukombozi wa Tigray, TPLF waliuteka mji huo Agosti mwaka huu, vikosi vya serikali vilikabiliana na waasi hao mwanzoni mwa Desemba na kulazimisha kuondoka.

Wiki iliyopita, wakazi waliripoti kwamba, wapiganaji wa Tigray walichukua tena udhibiti wa mji huo baada ya jeshi na washirika wake kujiondoa.

Rais wa Jimbo la Tigray, Debretsion Gebremichael, ameilaumu Uturuki, Iran na Falme za Kiarabu kwa kuuchochea mgogoro wa nchi hiyo kwa kutoa msaada wa kijeshi na kifedha kwa serikali.

Kituo cha televisheni cha Tigray, kilimnukuu Gebremichael akisema mgogoro wa sasa wa Ethiopia umechochewa na kuingiliwa kati kutoka nje.

Ndege za kijeshi zisizo na rubani za Ethiopia, zimeshambulia maeneo mbalimbali jimboni Tigray katika miezi ya hivi karibuni.

Serikali ya Ethiopia imewalaumu wapiganaji wa Tigray kwa kuwaua raia na kuharibu miundombinu katika maeneo yaliyokuwa chini ya udhibiti wao.

Kauli hiyo ya kiongozi wa jimbo la Tigray, imejiri wakati Waziri MKuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed akihudhuria mkutano wa tatu wa Uturuki na Afrika, mjini Istanbul akisifu mahusiano ya kihistoria kati ya nchi mbili hizo.

Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, lilipiga kura kuunga mkono kuundwa jopo la watalaamu watakao chunguza vitendo vya kukiukwa haki za binadamu katika vita vya nchini Ethiopia, vilivyoanza tangu Novemba mwaka jana.

Mzozo wa zaidi ya mwaka mmoja kati ya wapiganaji wa Tigray na vikosi vya serikali umesababisha vifo vya maelfu ya watu na kuwaacha maelfu ya wengine wakikabiliwa na baa la njaa. **DW**

# NABI AFUNGUKA UGUMU MECHI TANZANIA PRISONS

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Yanga, Nasreddine Nabi, amesema licha ya kupata pointi tatu ugenini katika mchezo wa wa Ligi Kuu dhidi ya Tanzania Prisons juzi, amekiri mechi hiyo ilikuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa.

**Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Nelson Mandela mkoani Rukwa, hivyo kuendelea kutawala kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 23 baada ya kushuka dimbani mara tisa.**

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Nabi alisema wachezaji wake walijitahidi kupambana licha ya baadhi yao kucheza wakiwa wagonjwa.

"Ninawapongeza wachezaji wangu kwa kazi nzuri waliyoifanya baada ya kupambana mpaka kuipa ushindi timu yetu, licha ya kwamba kulikuwa na wachezaji tisa ambao walikuwa wagonjwa, lakini wamepambana tukapata ushindi ugenini,"alisema Nabi.

Hata hivyo, alisema kipindi cha kwanza timu ya Tanzania Prisons ilipata nafasi moja na kuitumia vizuri kupata bao la mapema katika mchezo huo, lakini kipindi cha pili wachezaji wake walicheza vizuri na hatimaye kuondoka na pointi tatu.

Kocha huyo alisema alitambua mapema ugumu wa mchezo huo baada tu ya kuona hali ya baadhi ya wachezaji wake kutokuwa nzuri, na kuahidi mashabiki wao kuendeleza ushindani kwenye michezo yao yote ili kufikia lengo lao la kutwaa ubingwa msimu huu.

Kwa upande wa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingiza, alisema anafurahishwa na kiwango kinachooyeshwa na wachezaji wao katika michezo yao yote ya Ligi Kuu msimu huu.

Mtendaji huyo aliweka wazi suala zima la usajili wa wachezaji katika dirisha dogo ambalo lilifunguliwa tangu wiki iliyopita kuwa wana mpango wa kuongeza wachezaji haraka iwezekanvyo ili kuziba nafasi za wachezaji wao wenye majeraha ya muda mrefu.

"Dirisha la usajili bado halijafungwa tunaendelea kufanya mazungumzo na wachezaji ambao tunawahitaji kwa ajili ya kuiongezea nguvu timu yetu, tunahitaji kikosi kipana chenye ushindani mipango yetu ikikaa sawa tutawafahamisha mashabiki wetu nani na nani ambaye tumemchukua na wale ambao hatutaendelea nao," alisema Mazingiza.

Alisema Yanga ni klabu kubwa hivyo inahitaji wachezaji wenye viwango vya juu na si ili mradi mchezaji, hivyo mashabiki wao waendelee kuvuta subira katika kipindi hiki wanachoelekea kufanya usajili.

**ASANTE SANA...**




Kocha Mkuu wa Coastal Union, Melis Medo, akimshukuru shabiki wa timu hiyo aliyesafiri kutoka jijini Tanga hadi mjini Musoma mkoani Mara kwa ajili ya kuishangilia kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United uliopigwa katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Azam yataja siku ya 'majembe' mapya

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umesema Januari Mosi 2022, wataweka wazi majina na nafasi za wachezaji ambao watawasajili katika kipindi hiki cha dirisha dogo kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu hiyo.

Dirisha dogo la usajili limefunguliwa Desemba 16, mwaka huu na linatarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani. Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabiti 'Zaka Zakazi' (pichani chini), alisema mchakato wa usajili unaendelea vizuri na hawana haraka katika hilo.

Alisema hawawezi kuweka wazi nafasi na aina ya wachezaji watakaowasajili kwa sababu bado Kocha Abdihamid Moallin, akisaidiana na Mohammed Badru wanapitia ripoti ya mwalimu aliyeondoka George Lwandamina.

"Muda upo, ukizingatia makocha waliokuwapo wapitie kwanza ripoti ya kocha aliyepita (Lwandamina), kuangalia mapendekezo hayo na maoni yao kulingana na mahitaji ya timu, wapi kunatakiwa kuboresha na nani atakayeongezwa kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kikosi," alisema Zaka Zakazi.

Alisema kuhusu kurejeshwa kikosini kwa nyota wao watatu waliosimamishwa, Aggrey Morris, Mudathir Yahya na Salum Abuubakar, bado wanaendelea na adhabu hiyo hadi hapo bodi itakapokutana.

"Hakuna taarifa zozote za kurejea kikosini kwa nyota hao, bado wanaendelea kutumikia adhabu ya kusimimishwa kwa muda usiojulikana hadi hapo bodi itakapokaa na kujadili suala la wachezaji hao," alisema Zaka Zakazi.

Wakati nyota hao wanatumikia adhabu huku Mudathir akiwa amebakiza miezi sita, Aggrey na Sure Boy mikataba yao imebaki miezi nane ili ifikie tamati na kuwa wachezaji huru.

# Ben Pol kufunga mwaka na mashabiki wake

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva na R&B, Behman Paul 'Ben Pol', amejiandaa kufunga mwaka 2021 na mashabiki wake kwa kutoa burudani kabambe ya muziki sambamba na kupata nao chakula cha jioni, ameeleza.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Ben Pol ameweka wazi kuwa ikimpendeza Mungu kwa kumwezesha kufikia Desemba 31, mwaka huu, malengo yake ni kufunga mwaka na mashabiki wake na kufurahia pamoja kwa burudani kubwa ya muziki na chakula.

"Ninatarajia kuuaga mwaka 2021 na kuukaribisha 2022 kwa staili ya show kubwa ya muziki wa 'laivu' (mubashara) ambao utaambatana na urushaji wa mafataki kuukaribisha mwaka mpya," alisema.

Alisema 'shoo' hiyo inatarajiwa kufanyika wakati wa mkesha wa mwaka mpya Desemba 31, ambapo ataanza kwa kujumuika katika chakula cha jioni pamoja na mashabiki wake watakaohudhuria usiku huo, ambao pia utakuwa na michezo ya watoto, na muziki wa laivu ukiongozwa na yeye na bendi yake.

"Mashabiki zangu wamekuwa wakizipokea vizuri sana kazi zangu kwa muda mrefu sasa, nashukuru kwa upendo na sapoti kubwa wanayonipa, nina kila sababu ya kusherehekea kwa kujumuika nao kwa chakula na muziki mzuri wa 'live' kwenye mkesha wa mwaka mpya," alisema.

Aidha, Ben Pol alisema, asilimia 20 ya mapato atakayopata kwenye usiku huu, amepanga kuirudisha kwa jamii kwa kuwasaidia vifaa vya shule wanafunzi wanaoanza shule ya msingi mwaka 2022 waishio kwenye mazingira magumu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### HAALAND KUTUA MADRID

MKURUGENZI Mtendaji wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke amethibitisha kwamba, Real Madrid wana nia ya kutaka kumsajili, mshambuliaji wao, Erling Braut Haaland, 21. ***(Bild)***

#### MBAPPE NAE AWANIWA

REAL Madrid wanafikiria kuwaweka pamoja Erling Haaland na Kylian Mbappe, 22. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa anaweza kujadili mkataba wa awali na kupanga mpango wa kuondoka Paris St-Germain Januari. ***(Fichajes)***

#### SILVA KUPEWA MKATABA

KLABU ya Manchester City wako tayari kukamilisha maandalizi ya kumpatia mkataba mpya, Bernardo Silva, 27 raia wa Ureno. ***(Sun)***

#### POGBA BAIBAI UNITED

PAUL Pogba, 28, amecheza mechi yake ya mwisho kwa Manchester United na ataondoka kwenye klabu hiyo Januari. Real Madrid wamekuwa wakihusishwa na kiungo huyu wa kati Mfaransa ambaye mkataba wake unamalizika Juni. ***(Football Insider)***

#### AKATALIA FIORENTINA

MSHAMBULIAJI wa Fiorentina, Dusan Vlahovic, 21, ambaye amekuwa akihusishwa na klabu kama vile Manchester City, Arsenal na Newcastle, amekataa ofa ya hivi karibuni ya klabu yake. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

#### FERNANDINHO KUBAKI

KIUNGO wa kati Mbrazili Fernandinho, 36, anaonekana yuko tayari kuendelea kubaki Manchester City Januari, huku matumaini ya kuhamia Atletico Mineiro kwa mchezaji huyo yakififia.

#### TRIPPIER ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Atletico Madrid imemwacha mlinzi wa England, Kieran Trippier, 31, ahamie Newcastle kwa pauni milioni 15, iwapo wanaweza kusaini mkataba na mchezaji mwingine mbadala. ***(Mail)***

#### COUTINHO APEWA OFA

BARCELONA wamempa ofa kiungo wa kati Mbrazili Philippe Coutinho, 29, ya kuhamia klabu yoyote kati ya Tottenham na Newcastle. ***(Mirror, via Goal)***

#### CAVANI HUYOOO BARCA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Edinson Cavani, 34, ndiye anayelengwa na Barcelona kwenye dirisha la usajili la Januari, lakini Barca wanataka kuhakikishiwa kwamba raia huyo wa Uruguay amepona jeraha lake kabla ya kusaini mkataba. ***(Sport)***

#### PSG WAMTAKA GAVI

KLABU ya Paris St-Germain inajiandaa kujaribu nia yao ya kutaka kumsajili Gavi mwenye umri wa miaka 17. ***(El Nacional)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP ALIA NA MWAMUZI KUSHINDWA KUMTOA KANE

●●● Baadhi ya maswali pengine angeulizwa Mr. Tierney kwa kile anachofikiri...

**LONDON,** England

JURGEN Klopp amemshutumu mwamuzi, Paul Tierney kwa makosa ya kushindwa kumtoa nje Harry Kane na kukataa penalti ya Diogo Jota wakati Liverpool ikitoka sare na Tottenham juzi, Jumapili.

Kocha huyo wa Liverpool amesema mchezo huo ulihitaji "mwamuzi mwenye maono" - kauli ambayo inaweza kumweka kwenye matatizo.

"Sijui tatizo ni nini," alisema Klopp, ambaye alizungumza na mwamuziki kipindi cha pili na mwisho wa mchezo.

**Kocha huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, anaamini kuwa Kane alitakiwa kutolewa nje kipindi cha kwanza kwa kumchezea vibaya mlinzi wa kushoto, Andy Robertson, ambaye alitolewa nje dakika za majeruhi kwa kumfanyia faulo, Emerson Royal, wakati mchezo huo ukimalizika kwa sare ya mabao 2-2.**

Na Klopp hakuridhishwa kabisa na maamuzi ya Tierney kukataa kutoa penalti kwa Liverpool wakati Jota alipofanyiwa faulo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo ambao Klopp alipewa kadi ya njano, alisema: "Baadhi ya maswali pengine angeulizwa Mr. Tierney kwa kile anachofikiri." Alipoulizwa kuhusu faulo la Kane, ambayo ilimfanya straika huyo wa Tottenham kupewa kadi ya njano kwamba alitakiwa kupewa adhabu kubwa zaidi, Klopp alisema: "Kwa uhakika kabisa."

MECHI KALI
HOME
AWAY
SEVILLA FC
2.43 | 3.30 | 2.90
BARCELONA

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# POGBA, MAN UNITED BADO HAKIELEWEKI

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imebakiwa na wiki mbili tu za kufanya mazungumzo na kiungo wake, Paul Pogba kabla ya kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajiri la Januari ambapo atakuwa huru kuweza kufanya mazungumzo na klabu yoyote.

Man United hivi karibuni ilikuwa na mazungumzo ya kuwapa wachezaji wake mikataba mipya, lakini hawakuwa na mpango wa kuongeza mishahara na ilisababisha wengi kutoafiki makubaliano ikiwamo Pogba.

Kocha wa muda wa Man United, Ralf Rangnick amekuwa akiirudia kauli yake ya kutokuwa na msukumo wowote wa kumshawishi mchezaji yeyote ili aweze kusalia klabuni hapo.

Pia, alimruhusu Pogba kusafiri kwenda Dubai kwa ajili ya kujiuguza majeraha yake.

Kwa sasa Pogba amerudi Uingereza baada ya kuzungumza na kocha wake huku akiwa bado hafahamu hatima yake ndani ya klabu hiyo huku mkataba wake wa sasa ukiwa unaisha Juni mwakani.



# PSG bado yahaha kumbakiza Mbapp

**PARIS,** Ufaransa

MKURUGENZI wa michezo wa Klabu ya PSG, Leonardo amesisitiza kuwa wapo kwenye nafasi nzuri ya kuhakikisha kuwa mshambuliaji wao hatari, Kylian Mbappe anabaki klabuni licha ya kuwa mkataba wake unaisha majira ya joto.

Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ameifungia klabu hiyo mabao 145 kwenye michezo 194 katika mashindano yote tangu aliposajiliwa mwaka 2018 akitokea klabu ya Monaco kwenye usajili uliomfanya kuwa mchezaji ghali wa pili duniani wa muda wote.

"Ni suala muhimu sabal zungumzia mchezaji bora nia, ambaye mkataba wak wenda kuisha," alisema L akinukuliwa na Jarida la Football.

"Tunaweza kusema tu umza naye mara nyingi kw upole zaidi, lakini ndio seh kujenga mahusiano.

"Kuna gumu kidogo ila k na nyingine tungependa a kuwapo maisha yake yote pia itatupasa kuheshimu r familia yake, nadhani tu nzuri ya kuhakikisha anasa naamini hilo."

HABARI MICHEZO








MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 21 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1521 | Empoli Youth vs Sassuolo Youth | 1.72 | 3.85 | 3.85 |
| 14:30 | 1928 | Juventus Youth vs Cagliari Youth | 1.50 | 4.15 | 5.22 |
| 16:00 | 1530 | Smouha Club vs Ismaily SC | 2.43 | 3.06 | 2.96 |
| 16:30 | 2107 | Pescara Youth vs US Lecce youth | 3.46 | 3.84 | 1.82 |
| 16:30 | 2391 | Bologna Youth vs AC Milan Youth | 3.03 | 3.56 | 2.04 |
| 17:00 | 1883 | Antalyaspor vs Kasimpasa | 2.03 | 3.41 | 3.46 |
| 17:00 | 4561 | Northeast United FC vs ATK Mohun Bagan | 3.08 | 3.42 | 2.07 |
| 17:00 | 4971 | Basaksehir vs Giresunspor | 1.74 | 3.65 | 4.44 |
| 18:30 | 3071 | Pyramids vs Talaea El Gaish | 1.33 | 4.93 | 8.28 |
| 20:00 | 1317 | Altay vs Trabzonspor | 3.49 | 3.59 | 1.96 |
| 20:00 | 2052 | Adana Demirspor vs Galatasaray | 3.06 | 3.40 | 2.20 |
| 20:00 | 2948 | Hapoel Katamon vs Nazareth Ilit | 2.94 | 2.98 | 2.36 |
| 20:15 | 3942 | Maccabi Netanya vs Hapoel Haifa | 2.42 | 3.15 | 2.71 |
| 20:30 | 2241 | Udinese vs Salernitana | 1.42 | 4.60 | 7.20 |
| 20:45 | 3414 | FC Ashdod vs Hapoel Tel Aviv | 2.36 | 3.08 | 2.84 |
| 20:45 | 4519 | Vitesse Arnhem vs PEC Zwolle | 1.45 | 4.41 | 6.08 |
| 21:00 | 1970 | Arab Contractors vs Zamalek | 7.11 | 4.15 | 1.44 |
| 21:00 | 5094 | Villarreal vs Alaves | 1.45 | 4.40 | 7.00 |
| 21:30 | 4903 | Maccabi Haifa vs Hapoel Hadera | 1.23 | 5.19 | 10.57 |
| 21:45 | 5711 | Tondela vs GD Estoril | 3.00 | 3.19 | 2.21 |
| 22:00 | 5282 | Tranmere vs Harrogate | 2.14 | 3.23 | 3.09 |
| 22:45 | 1135 | Hayes Yeading United vs Salisbury City | 1.42 | 4.53 | 5.78 |
| 22:45 | 1219 | Juventus vs Cagliari | 1.24 | 5.84 | 12.40 |
| 22:45 | 1246 | Taunton Town vs Harrow Borough | 2.01 | 3.53 | 3.14 |
| 22:45 | 1647 | Guingamp vs Dunkerque | 1.94 | 3.29 | 3.83 |
| 22:45 | 1664 | Nantwich Town vs Lancaster City | 2.56 | 3.42 | 2.40 |
| 22:45 | 2260 | Nancy vs Dijon | 2.81 | 3.00 | 2.56 |
| 22:45 | 2569 | Stirling vs Elgin City | 2.16 | 3.26 | 3.02 |
| 22:45 | 2635 | Paris FC vs Amiens | 1.85 | 3.24 | 4.32 |
| 22:45 | 2693 | US Quevilly Rouen vs Caen | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 22:45 | 2698 | AC Ajaccio vs Grenoble Foot | 1.71 | 3.34 | 5.11 |
| 22:45 | 2936 | Niort vs PAU FC | 2.50 | 3.18 | 2.74 |
| 22:45 | 3329 | Kettering Town vs Southport | 1.86 | 3.53 | 3.57 |
| 22:45 | 3420 | Cheshunt vs Bowers Pitsea | 1.58 | 3.87 | 4.83 |
| 22:45 | 3434 | Telford vs Guiseley | 2.24 | 3.32 | 2.84 |
| 22:45 | 3484 | Nimes vs Toulouse | 3.43 | 3.33 | 2.05 |
| 22:45 | 3540 | Sochaux vs Valenciennes | 1.87 | 3.30 | 4.13 |
| 22:45 | 3671 | Bradford PA vs Halifax | 4.15 | 3.57 | 1.73 |
| 22:45 | 3863 | Genoa vs Atalanta | 6.40 | 4.90 | 1.43 |
| 22:45 | 4175 | Gainsborough vs Hyde United FC | 2.23 | 3.47 | 2.75 |
| 22:45 | 4447 | Dungannon Swifts vs Warrenpoint | 1.89 | 3.81 | 3.23 |
| 22:45 | 4710 | Rodez Aveyron vs Bastia | 2.38 | 3.05 | 3.20 |
| 22:45 | 4814 | Yate Town vs Farnborough Town | 2.75 | 3.56 | 2.20 |
| 22:45 | 4979 | Linfield Belfast vs Ballymena Utd | 1.29 | 4.99 | 8.25 |
| 22:45 | 5262 | Peterborough Sports vs Banbury United | 1.86 | 4.00 | 3.65 |
| 22:45 | 5558 | AJ Auxerre vs Le Havre | 2.06 | 3.19 | 3.54 |
| 22:45 | 5723 | Arsenal vs Sunderland | 1.21 | 5.94 | 12.23 |
| 23:00 | 5705 | AZ Alkmaar vs Groningen | 1.33 | 4.80 | 8.23 |
| 23:30 | 5768 | Sevilla FC vs Barcelona | 2.43 | 3.30 | 2.90 |
| 23:45 | 3692 | Famalicao vs Portimonense | 2.20 | 3.18 | 3.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SIMBA YAKOSHWA NA KASI UCHANGIAJI UJENZI UWANJA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeonyesha kufurahishwa na kasi ya michango inayotolewa na wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kwa ajili ya ujenzi wa uwanja ambao itakuwa inautumia kucheza mechi zake za nyumbani kwenye michuano ya ndani na kimataifa.

**Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, amesema kutokana na wanachama na mashabiki kuonekana kuitikia wito huo kwa wingi, ana imani kuwa lengo lililokusudiwa litatimia.**

"Tunaendelea na michango vizuri tu, natumai tutafikia malengo tuliokusudiwa, na tunawaahidi wanachama na mashabiki wa klabu yetu kuwa tutakuwa tunatoa taarifa ya michango hiyo, na tutakuwa wawazi kwenye mipango na matumizi ya fedha hizi kutoka kwao," alisema.



Kiasi cha wiki moja sasa, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wamekuwa kwenye zoezi la kuchangia pesa kwa ajili ya uwanja ambao itautumia kwenye mechi zao za kimashindano.

Wengi baada ya kuchanga, wamekuwa wakitoa nakala ya miamala kwenye mitandao ya kijamii hasa ya michezo, kwa ajili ya kuhamasishana.

Wazo hilo lilianza kutolewa na baadhi ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwenye mitandao ya kijamii baada ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez, kuzuiwa kuingia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuangalia mechi ya timu yake ikicheza dhidi ya Yanga Desemba 11, mwaka huu.

Baada ya wazo hilo, Mshauri wa Mwekezaji wa klabu hiyo, Crescentius Magori, aliunga mkono wazo hilo na kuongeza kuwa imefika wakati sasa wa kukataa tukio alilofanyiwa Ofisa Mtendaji Mkuu huyo kwa vitendo na si maneno kwa kuchangia kupata uwanja wenye uwezo wa kuingiza angalau mashabiki 30,000.

Mohamed Dewji, Mwekezaji na Rais wa Heshima wa klabu hiyo, alikubaliana na wazo hilo na kuishauri Bodi ya Wakurugenzi kutoa utaratibu wa michango, huku mwenyewe akiahidi kuchangia shilingi bilioni mbili.



# Sure Boy, Yanga sasa mambo safi

**Na Dennis Fussi**

TAARIFA za ndani kutoka Klabu ya Yanga zinapasha kuwa kiungo, Salum Abubakar 'Sure Boy' amefanya makubaliano ya awali ya kuitumikia miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam.


Sure boy amesimamishwa na klabu yake kwa muda usiojulikana sambamba na kiungo mwenzake mkabaji, Mudathir Yahaya na beki mkongwe na nahodha wao mkuu, Aggrey Morris kwa utovu wa nidhamu.

Hata hivyo, taarifa kutoka ndani ya Azam zimebainisha kuwa, Morris na Yahaya wamerudishwa kikosini, huku Sure Boy akikataa kwa madai kwamba, hajaambiwa kosa lake.

Taarifa za awali zilieleza kwamba, wachezaji hao wameishtaki klabu yao kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kufuatia adhabu yao ya kusimamishwa kwa muda usiojulikana.

Mmoja wa viongozi wa Yanga ambaye hakuwa tayari kulitaja jina lake ameliambia gazeti hili kuwa Sure Boy amefanya vikao mara mbili na mabosi wa Yanga kabla ya kukubali kuwa tayari kusaini mkataba wa miaka miwili, lakini anasubiri kwanza hatima yake ndani ya Azam FC.

Ndani ya Azam kulifanyika kikao kizito katika kujadili wachezaji hao, lakini mabosi waliweka ngumu wachezaji hao kurejeshwa wakihofia kutibua zaidi nidhamu kwa wenzao.



e

bu tuna-
wa du-
ke unak-
eonardo
France

mezung-
a njia ya
nemu ya

wa nam-
endelee
hapa na
nafasi ya
nanafasi
lia hapa,

# Michezo

Jumanne Desemba 21, 2021

Nipashe




## Pogba, United bado hakieleweki

UKURASA 22

**TUMEREJEA...**



Wachezaji wa Simba, Jonas Mkude (kushoto) na Hassan Dilunga, ni miongoni mwa kikosi cha wachezaji 23 ambao walisafiri na timu kwenda Bukoba kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, ambayo hata hivyo haikuchezwa kutokana na nyota wengi wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao kuugua. **PICHA: MAKTABA**

## FCC yaita faili nyaraka za mkataba TFF, GSM

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Ushindani (FCC) imeagiza kupewa nyaraka za mkataba wa udhamini wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Shirikisho la Soka (TFF) na Kampuni ya GSM.

Novemba 23, mwaka huu, Kampuni ya GSM iliingia mkataba wa miaka miwili na TFF kuwa mdhamini mwenza wa Ligi Kuu Tanzania Bara wenye thamani ya Sh. bilioni 2.1, ambao uliibua mvutano baada ya uongozi wa Klabu ya Simba kupinga kuvaa jezi zenye nembo ya mdhamini mwenza huyo.

Mwishoni mwa wiki, TFF ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari, ikibainisha kuwa Bodi ya Ligi Kuu (TPLB) ilikutana na klabu 16 zinazoshiriki ligi hiyo na kwamba 15 kati yake zimeridhia udhamini huo wa GSM.

Wakati hayo yakifanyika, jana katika semina ya wahariri wa habari za biashara, Ofisa Mawasiliano wa FCC, Wilfred Nsajigwa, alisema wanafuatilia suala hilo kwa mujibu wa sheria.

Alisema hatua ya kwanza iliyochukuliwa ni kuagiza kupewa nyaraka za mkataba huo ili kujiridhisha kama matakwa ya kisheria wanayoyasimamia yamezingatiwa ama la.

"Tumewataka TFF watupatie nyaraka za udhamini huo unaolalamikiwa. Tukishazipata, tutaangalia vitu vyote, ili tufanye uamuzi ni lazima tupate nyaraka. Kazi hii haifanywi na mtu mmoja. Ndani ya tume tuna tume ya kushughulikia masuala haya inayoundwa na wajumbe watano, mimi nikiwamo," alisema.

# Pablo apewa rungu Simba

## ●●● Watua kimyakimya kambini, ripoti ya daktari yaichelewesha kuiwinda KMC FC, huku...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kimewasili jijini Dar es Salaam juzi usiku kimyakimya kutoka Bukoba na kuelekea kambini huku wachezaji wao wakienda moja kwa moja kufanyiwa vipimo vya afya, uongozi wa klabu hiyo kwa sasa unasubiri ripoti ya Kocha Mkuu, Pablo Franco kupendekeza maeneo anayohitaji kuboreshwa.

**Jumamosi iliyopita Simba ilishindwa kucheza mechi yake ya Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba baada ya wachezaji wake 16 kuugua mafua na kukohoa na homa, (Season Influenza) hali iliyoelezwa ni kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.**

Hata hivyo, juzi timu hiyo ilirejea Dar es Salaam kimyakimya na kuingia kambini moja kwa moja tayari kujiandaa na mechi ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayopigwa Desemba 24, mwaka huu, katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Thierry Hitimana, alisema baada ya kurejea juzi usiku wachezaji wote wameingia kambini na jana kupatiwa vipimo kwa ajili ya kuangalia afya zao kuelekea mechi ijayo dhidi ya KMC FC.

Alisema hali ya wachezaji wao haiko sawa na hawataendelea na mazoezi hadi hapo watakapopata majibu ya vipimo ili kugundua tatizo na baada ya hapo ndipo wataendelea na programu zao.

"Tumeingia jana (juzi) usiku Dar es Salaam, wachezaji wote wako kambini na hatuwezi kuendelea na programu ya mazoezi hadi hapo tutakapopata majibu ya vipimo kuona tatizo la wachezaji wetu, baada ya hapo tutaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo ujao," alisema Hitimana.

Kuhusu usajili, Hitimana alisema hadi sasa hakuna mapendekezo yoyote yaliyotolewa kutoka benchi la ufundi, na kwamba viongozi wanasubiri ripoti kutoka kwa Pablo ili kuanza kuboresha timu yao.

Alisema bado hawajakaa na bosi wao (Pablo) kupitia ripoti na ana imani kila kitu kitakuwa sawa kwa sababu muda wa kufanya usajili bado upo hadi Januari 15, mwakani.

Naye Mwenyekiti wa Wanachama wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, alisema wako makini katika kila kitu na suala la usajili wanasubiri ripoti kutoka benchi la ufundi linaloongozwa na Pablo.

Alisema watafanya maboresho kwa kusajili wachezaji kulingana na mahitaji ambayo yanapendekezwa na kocha wao huyo kwa ajili ya michezo iliyopo mbele yao ikiwamo kutetea ubingwa wao na kufikia malengo yao kwa msimu huu.

"Tutafanya maamuzi magumu katika dirisha dogo la usajili kupata wachezaji bora kama ambavyo kocha (Pablo) atahitaji kwa ajili ya kuifikisha timu yetu katika malengo ya kufanya vizuri na kutwaa makombe katika mashindano ya ndani na nje ya Tanzania," alisema Mangungu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >